# *Kumwamsha Yesu*

Habari za jioni. Kama kawaida, majaliwa kuwa katika nyumba ya Bwana.

2 Jinsi nilivyoshangaa kumwona mvulana huyu hapa kutoka Arkansas, rafiki yangu. Muda mrefu, ninaamini mara ya mwisho nilipokuona ilikuwa ni huko California, sivyo? Jamani, jamani! Ungali California? Hapa? Jamani! Nafikiri itanibidi kuhama. Mashariki yote inakuja magharibi.

3 Basi, vema, kila mtu ana furaha? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hiyo ni sawa.

4 Vema, nafikiri hii ni karibu ibada yetu ya sita sasa. Inatubidi kuendelea juma lijalo lote, na—na kuendelea mpaka Jumatatu ijayo usiku. Sasa, msisahau Jumatatu usiku huko Tucson, ile dhifa, nasi tunatarajia wakati mzuri sana kule chini Jumatatu hii ijayo usiku.

5 Nilikuwa nikizungumza na Ndugu Williams and Ndugu Rose, leo hii. Na kwa hiyo nikasema, "Mnajua, nitaanza kuwaombea wagonjwa." Nikasema, "Ninawaweka maskini watu hao kule kila usiku mpaka yapata saa nne ama tano." Nikasema, "Ninajisikia kuaibika sana kwa nafsi yangu, kwa kulifanya namna hiyo." Nami ninaomba msamaha kwa kuwaweka muda mrefu hivyo, bali sipati kuwaona mara nyingi sana.

6 Na siwezi kutoa udhuru huo, maana nafanya vibaya kuliko hivyo nyumbani. Mnaona? Wakati mwingine ninaanza asubuhi, mapema, na kuhubiri mpaka alasiri hiyo na wakati fulani, ama wakati wowote tunapokuwa tayari kwenda nyumbani. Nasi tunaketi tu huku, namna hiyo, tumesongamana tu tuwezavyo kuwa, kwa hiyo tunakuwa tu na wakati mzuri.

7 Ni vema kuwa hapa, Ndugu Groomer. Ambapo. . .[Mtu fulani anazungumza na Ndugu Branham—Mh.] Naam. Naam. Ilikuwa kidogo imefichika kwangu. Haikuwa. . .Nilikuwa hapa mwaka jana tulipokuja huku, sivyo? ["Naam."] Nilifikiri hivyo. Nakumbuka mahali hapa pamoja na kanisa. Nina furaha sana kuwa hapa usiku wa leo! Mungu awabariki ninyi nyote.

8 Na sasa tunamtarajia Bwana ku—ku—kuwaponya wagonjwa usiku wa leo. Kwa namna fulani tumeibadilisha ratiba kidogo, nami nitaingia kwenye Ujumbe, wa kuihubiri Injili, ama yale ninayojaribu kuwazia, kadiri nijuavyo mimi. Halafu basi ni—nikianza, sijui kabisa wakati wa kusimama. Ninaendelea tu, na kuwaweka muda mrefu sana. Halafu, nilidhani ungekuwa ni wakati mzuri usiku wa leo, baada ya siku nyingi usiku za kuhubiri, kujaribu tu sasa na kuwaombea wagonjwa. Kwa hiyo leo hii kwa namna fulani tumejiandaa kwa ajili yake na

kumngojea Bwana. Nami nilianza kuona jana usiku, jinsi. Kwa namna fulani inakubidi kwenda jinsi Yeye anavyokuongoza kwenda, mwajua. U—unasikia kitu kikikusukuma, na moja kwa moja maono yatatokea, nawe unajua ni jambo fulani linalokaribia basi.

9 Halafu, leo hii nilikuwa nikitoka, pia, katika. . . Nilikuwa kwenye. . . hoteli yangu, ndipo Roho Mtakatifu akasema niende njia fulani. Basi palikuwapo na kidimbwi cha kuogelea huko nje. Nilifikiria labda huenda mtoto mdogo amezama. Nikavuka pale, ikawa niliangalia pale, ndipo nikaona watu fulani. Wameketi hapa mbele usiku wa leo. Wanajua jinsi huyo alikuwa ni Bwana Ambaye alifika pale, na yale tu aliyosema hakika ndivyo lilivyo. Kwa hiyo nikajua basi ulikuwa ni wakati wa kuwaombea wagonjwa.

10 Na sasa tutamkaribia Yeye sasa, kwa maombi, kabla hatujalikaribia Neno Lake. Nanyi ni kusanyiko zuri sana. Mmekuwa wasikivu sana kila usiku. Ninajua baadhi yenu inawabidi kuamka na kuondoka wakati mwingine, kabla. Ninajua hiyo si kwa sababu mnataka tu kutoka nje. Inawabidi kuwahi mabasi. Inawabidi kwenda kazini. Na—natambua hilo.

Basi sasa hebu na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda mfupi tu sasa kwa ajili ya maombi.

11 Sasa, naona kuna wengi tu waliosimama huko nyuma kadiri ya wale wanaoketi hapa. Nasi tunataka. . . Tunajua kwamba Mungu atajibu maombi yao kadiri tu afanyavyo mahali popote. Sasa una haja? Acha ijulikane kwa mkono ulioinuliwa. Mungu atasikia.

12 Baba yetu wa Mbinguni, tunakuja sasa katika Uwepo wa Yesu, katika—katika Jina Lake. Nasi tunaenda kwenye kiti cha enzi cha neema, kuomba msamaha wa dhambi zetu, maana, tukijua, siku baada ya siku sisi tunakukosea. Kila saa ya maisha yetu, karibu hakuna moja inayopita pasipo sisi kulazimika kusimama, kusema, "Bwana, nisamehe. Si—sikumaanisha kulifanya tu jinsi hiyo. Ilinipasa kulifanya kwa njia hii—hii nyingine." Ndipo, tunajua, Bwana, kwamba Wewe daima umejaa rehema na tayari kuwasamehe watoto Wako. Unasikiliza kilio chao kilicho dhaifu sana. Tuna furaha sana kwamba tunaye Mtetezi.

13 Nasi tunaomba, Baba, usiku wa leo, kwa ajili ya kanisa hili, kwa ajili ya ndugu yetu mpendwa. Miaka hii yote huku, kumjua, na kumwona, tabia yake, mtumishi mzuri sana wa Kristo. Jinsi tunavyokushukuru Wewe kwa ajili ya mtu kama huyo! Mimi. . . Ni majaliwa makubwa mno, Bwana, kuwa miongoni mwake na watu wake, na kushirikiana nao, na kukusanyika pamoja kushiriki pamoja nao, kwenye Neno la Mungu. Tunaomba, Bwana, ya kwamba utatenda kazi kiajabu, usiku wa leo, na uta—na utatupa baraka hizi. Nina furaha sana kukutana na marafiki

wa kale ambao niliwajua miaka mingi iliyopita mwanzoni mwa huduma.

14 Na sasa, Bwana, tunaomba pamoja ya kwamba Wewe utatubariki kwa kuwa tulikusanyika pamoja usiku wa leo katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu. Tumekusanyika kwa kusudi hilo, Bwana, nasi tunaomba kwamba—kwamba Wewe utakidhi mahitaji yetu usiku wa leo, na kujibu maombi yetu Kwako, kuwaponya wagonjwa, kuwaokoa waliopotea, na kuwatia moyo waliovunjika moyo. Tunaomba katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

15 Sasa, tunawatakeni, mnaotaka, mnaopenda, usiku wa leo, kulifungua Neno la kale lililobarikiwa, katika kitabu cha Injili ya Mathayo Mtakatifu, mlango wa 8. Nasi tunataka kuanza kusoma kutoka kwenye... Tukiketi leo, kutoka Mathayo, mlango wa 8, kuanzia kifungu cha 23.

16 Baada ya kuondoka leo, kutoka kwa Ndugu... ama Ndugu Williams na Ndugu Jewel Rose kuachia mahali tulipokuwa, mimi... akili yangu iliangukia kwenye wakati mmoja maalum. Na kwa hiyo nikachukua tu... Kwa sababu, tulikuwa tukizungumza, na Roho Mtakatifu alikuwa ametukaribia sana. Kwa hiyo wakati tu wakiondoka, niliwaza, "Loo, jamani! Sasa Yeye hakika atanena." Basi nikachukua niani mwangu tukio fulani katika Biblia lililotukia, upesi nikaliendea. Nami nina Maandiko machache ya kuambatana nalo, na kutoa somo kwake, niliandika muhtasari kidogo juu yake. Ningetaka kuwaleteni haya.

17 Kwanza, hebu tusome sasa katika Mathayo Mtakatifu, mlango wa 8, na tuanzie kwenye kifungu cha 23.

> *Akapanda chomboni, wanafunzi wake wakamfuata.*
>
> *Na, tazama, kukawa msuko-suko mkuu baharini, hata chombo kikafunikizwa na... mawimbi, naye alikuwa amelala usingizi.*
>
> *Wanafunzi wake wakamwendea, wakamwamsha, wakisema, Bwana, tuokoe: tunaangamia.*
>
> *Akawaambia, Mbona mmekuwa waoga, Enyi wa imani haba? Mara akaondoka, akazikemea* upepo *na bahari; kukawa shwari kuu.*
>
> *Wale watu wakamaka, wakisema, Huyu ni mtu wa namna gani, hata* upepo *na bahari* humtii!

18 Hilo ni fungu dogo la kuvutia sana, ama Andiko. Nitachukua somo la kipekee kutoka kwake: *Kumwamsha Yesu. Kumwamsha Yesu.*

19 Hapana shaka ilikuwa ni si—siku ngumu sana Kwake. Alikuwa amechoka. Mwili Wake ulikuwa umedhoofika. Mwajua, wakati akienda, watu walimvuta Mungu kutoka Kwake. Walivuta shauku zao kutoka Kwake. Basi walipofanya hivyo...

Hatutajaribu kuingia kwa undani kuelezea hilo, kwa sababu hakuna mtu anayeweza kulielezea. Tunawezaje kuyaeleza mambo tusiyojua?

20 Hiyo ndiyo sababu hakuna njia, hata kidogo, ya kuokoka kamwe mpaka uwe tayari kuyakubali yale usiyoweza kueleza. Unaona? Huna budi kuamini. "Yeye amjiaye Mungu lazima aamini kwamba Yeye yuko." Sasa, hakuna njia ya kuthibitisha hilo kisayansi, bali huna budi kuliamini hata hivyo. Na kama ungeweza kulithibitisha, basi lisingekuwa ni tendo la imani tena. Nayo imani . . . Mungu amejificha sana hata inakubidi kuamini ya kwamba Yeye yupo, pasipo kumwona Yeye, ujue kwamba Yeye yupo, kwa vyovyote vile. Kwamba unaliona, ama hulioni, unaliamini. Hakika unaamini, kwa vyovyote vile.

21 Sasa, nafikiri hiyo ni ajabu sana, na hiyo inawapa wasio na elimu kama mimi nafasi, kila mtu, kuliamini, kwa sababu tunalisikia. "Nayo imani chanzo chake ni kusikia, na kusikia Neno la Mungu." Ndipo tunalikubali Hilo, na kuliamini Hilo. Na juu ya msingi wa imani yetu katika Hilo, tunaokoka, tunaponywa. Na chochote cha zaidi tunachovuta kutoka kwa Mungu, kinatoka kwenye Rasilimali isiyoonekana.

22 Wakristo; silaha zote za Ukristo ni imani. Kila kitu tulicho nacho hakionekani. Vitu pekee vilivyo halisi ni vile visivyoonekana, visivyoelezeka. Vitu vinavyoweza kuelezeka si vya halisi. Ni vya juujuu na hufa. Lakini mambo yasiyoweza kuelezeka hayafi, milki nzima. Tazameni silaha za Ukristo. Upendo, ni sehemu yako gani iliyo upendo? Upendo, furaha, imani, uvumilivu, upole, subira. Mnaona? Hakuna moja ya mambo hayo, huwezi kuyaona. Hayaonekani, lakini hata hivyo tunayaamini. Upendo kamwe haufi. Imani ndi—ndiyo ushindi. Tunaamini mambo tusiyoyaona.

23 Sasa, ndani ya Yesu mlikuwamo Mungu. "Mungu alikuwa ndani ya Kristo, akiupatanisha ulimwengu kwa nafsi Yake." Nao hawa watu waliamini ushuhuda Wake. Na wale ambao kweli waliuamini, wangeweza kuvuta baraka za Mungu kutoka Kwake. Basi walipofanya hivyo, Yeye alisema, "Nguvu zilimtoka." *Nguvu* ni "uweza." Yeye . . . Kwa maneno mengine, kama tungeweza kulisema leo hii: Yeye alidhoofika wakati watu walipovuta kutoka Kwake. Vema, kama ilitenda kazi hivyo katika mwili huo wa binadamu, itatenda kazi katika mwili mwingine wa binadamu.

24 Nasi tunajiumbia mazingira yetu kutuzunguka, kila mmoja wetu. Umekuwa na watu waliokuwa ni watu wazuri, bali ni vigumu tu kwako kuwa karibu nao. Halafu umekuwa na watu wengine ambao unapenda tu kuwa karibu nao. Unaumba mazingira hayo. Na, loo, hivi si ungalipenda kuwa karibu na Yesu kidogo tu? Ajabu! Uone jinsi hayo mazingira aliyoumba yangalikuwa, nakisia lilikuwa ni lundo moja kubwa tu la

upendo, heshima, na kicho cha kitauwa. Sasa, mara nyingi nimewasikia watu wakisema. . .

25 Wengi wenu, nadhani, tayari mmeicheza kanda ya lile ono la mwisho huko juu, sababu ya mimi kuwa papa hapa Arizona sasa. Na hiyo ilikuwa. . .Loo, jamani! Mkiipata, ni, *Bwana, Ni Wakati Gani?* Basi ukiipata, kama ulipata kununua kanda kutoka kwetu, ipate hiyo. Sasa, hizo si zangu. Ni mali ya kampuni nyingine iliyo pamoja nasi, ya kanda, nazo si zangu. Kwa hiyo, lakini, ninajua mvulana huyo anazo.

26 Nami sijawahi kuwa na kitu kama hicho kilichopata kutukia. Baadhi yao husema, "Unapokuwa katika Uwepo wa Mungu, kwa nini usimuulize *hili* ama *lile*?" Ni—ni tofauti na vile wewe. . .Unaona, kile watu wengi wanachokiita nguvu za Mungu, ni baraka tu za Mungu. Nguvu za Mungu kwa jumla ni tofauti na baraka za Mungu. Nguvu za Mungu, katika Uwepo Wake, kamwe hujui la kufanya. Unaninii tu. . .Wewe ni—wewe unaninii sana. . .Unaogopa sana hata unaingia ganzi, mwili mzima.

27 Kuna siku mbili, hata mgongoni mwangu na nyuma ya kichwa changu, na huku na huku mwilini mwangu, nisingeweza kuhisi, hata kidogo. Na kuingia ganzi kabisa, pamoja na hofu kuu, wakati lile kundi la Malaika lilipokuwa limesimama papa hapa, sasa, kusimama tu, nikiwaangalia kama nilivyo sasa.

28 Na kama unafikiria hilo lingekuwa, "Loo, vema"? La. Kama wewe uko pale kweli na kuliona, ni tofauti.

29 Na sasa, Bwana Yesu, akiwa ni Imanueli, hapana shaka alikuwa amechoka. Nguvu zilimtoka. Naye alikuwa na kazi kubwa mbele Yake, siku iliyotangulia, wakati aliposhuka upande wa pili, kama sote tujuavyo, maana Yeye alivuka kwenda Gadara, na huko ndiko alikokutana na huyu mwendawazimu. Yeye aliwazia, labda, wakati hicho chombo kilipokuwa kikivuka Galilaya, ambacho labda kilichukua muda mrefu kidogo, Yeye alichukua tu fursa ya hiyo nafasi kupumzika kidogo. Hilo si zaidi ya—ya kawaida, kile mtu yeyote angalifanya.

30 Walikuwa wameingia ndani ya chombo pamoja na Yeye, na wakamwingiza chomboni. Nao walikuwa wamevuka bahari, kuhubiri ng'ambo ya pili. Ndipo Yesu akaona nafasi hii adhimu, akiwa mchovu na mnyonge, kwa sababu Yeye alikuwa ni mwanadamu. Hakuwa asiyepatikana na mauti wakati huo. Alikuwa ni Mwanadamu, na ilimbidi kufa. Hiyo ndiyo sababu ilibidi Mungu kufanyika Mtu, apate kufa. Sasa, Huyo hapo, na ni mzito wa macho na mchovu. Wanafunzi Wake wakachukua makasia wakaanza safari.

31 Katika siku hizo, walikuwa, kama walikuwa na upepo wowote, wangeibisha meli na—na ingeweza kuendeshwa kwa matanga. Na wakati mwingine kama ilikuwa inaenda polepole sana, hata hivyo ilisaidia kidogo, kwa kuvuta makasia,

wangeyachukua makasia na kuyatumia kuendelea. Na kwa matanga, pia, wangeweza kuwa na wakati mzuri sana. Mmoja aliketi nyuma. Kwa kawaida, katika meli kubwa kama hiyo, yapata watu wanane ama kumi kuvuta makasia. Vema, walikuwa na u—usukani, na mtu mmoja alishughulikia huu usukani, huko nyuma, kama ilikuwa ikiabiri. Halafu, kama ilikuwa ni kuvuta makasia, hakika, wangeweza kuufunga usukani na kuvuta makasia yao.

32 Sasa, hebu tuwazie tu walikuwa wamepandisha matanga juu, maana hapana shaka kulikuwako na upepo mdogo ukivuma, kutokana na yale yaliyotukia baada ya kitambo kidogo. Na mtu yeyote anajua, sehemu hiyo ya Galilaya, ama huko chini, loo, jamani, lolote laweza kutokea wakati wowote. Na kwa hiyo walikuwa wakienda zao, wakiabiri kuvuka pale.

33 Basi hapana shaka Yesu alikuwa ameenda upande wa nyuma wa maskini chombo hicho, akajikunja, kisha akajilaza katika lundo dogo kule nyuma, apate tu kupumzika na kurudisha nguvu kutokana na kupoteza Kwake nguvu, kwa ajili ya ibada Yake iliyokuwa inamngojea.

34 Basi hapana shaka hao wanafunzi walikuwa wakishangilia mmoja kwa mwingine, juu ya yale waliyokuwa wakimwona akitenda. Hapana shaka ulikuwa ni wakati mzuri sana kwao, maana walikuwa—walikuwa na wakati, wakishuhudiana labda mmoja na mwenzake. Na labda walikuwa wakijadiliana juu ya baadhi ya mambo waliyokuwa wamemwona akitenda.

35 Na sasa hebu tusimame hapa kwa dakika moja tusikilize majadiliano yao. Huenda walijadiliana ma—mahali ambapo Yeye alikuwa amesema kitu kama hiki, "MIMI NIKO AMBAYE NIKO." Wakati Yeye aliposema . . .

Walisema, "Baba zetu walikula mana nyikani, nao walikuwa chini ya Musa."

36 Naye Yesu akasema, "Nao, kila mmoja wao, wamekufa." Kuna wawili tu waliofaulu kuingia katika nchi ya ahadi, mnaona, Yoshua na Kalebu. "Wote wamekufa. Lakini Mimi ndimi Mkate wa Uzima ulioshuka kutoka kwa Mungu, kutoka Mbinguni. Mtu anaweza kula Mkate huu na asife." Akabadilisha, ilikuwa ni tofauti. Angewezaje Yeye kuwa ni Mkate? Huenda walipitia hayo. Na huenda walipitia . . .

37 Kwa kuwa labda kuna wageni hapa, kwa ajili ya ibada ya uponyaji, huenda nikasema hivi. Huenda walisema . . . Sasa, hilo lingekuwa ni jambo moja ambalo Yeye alidai, ya kwamba Yeye alikuwa yule "MIMI NIKO" aliyekuwa kwenye kichaka kilichowaka moto. Maana, walisema, "Wewe ni mtu asiyezidi miaka hamsini nawe unasema umemwona Ibrahimu. Sasa tunajua Wewe una kichaa." Mnaona, *kichaa* linamaanisha "wazimu." "Nawe hujapita bado miaka hamsini," wakati Yeye alikuwa na thelathini tu. "Lakini," kasema, "Wewe una umri wa

karibu miaka hamsini tu, na wewe—wewe ulisema umemwona Ibrahimu? Sasa tunajua una kichaa." Unaona?

38 Lakini Yeye akasema, "Kabla ya Ibrahimu kuwapo, MIMI NIKO." Loo, jamani! Si tu kumwona Ibrahimu, bali, "Kabla ya Ibrahimu kuwapo, MIMI NIKO." Naye ni "MIMI NIKO" tu sasa kadiri alivyokuwa wakati huo. Sasa, kumbukeni, "MIMI NIKO" si "Nilikuwako," ama "Nitakuwako." "MIMI NIKO" ni sikuzote, wakati wote; yeye yule jana, leo, na hata milele. "MIMI NIKO."

39 Halafu basi huenda walisema, "Vema, sasa, hii hapa sababu moja tunayojua ya kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Kwa sababu, Yeye. . . Tunajua." Sasa, Yeye alikuwa tayari ameenda kulala sasa. "Nasi tunajua ya kwamba Yeye hana budi kuwa ni Masihi, kwa sababu tunaambiwa na Maandiko yale Masihi huyu atakayofanya hapo atakapokuja." Sasa, hiyo ni falsafa nzuri kwa mtu yeyote, na fundisho zuri, sahihi, kamili.

40 Hilo ndilo nililokuwa nikijaribu kufikia jana usiku, huko kwingine, Mesa. Sikuzote, usihukumu kwa mhemko. Hukumu kwa Neno. Inabidi iwe ni Neno. Sasa, angalieni Neno na kile Neno lisemacho, ndipo mjue kwamba ni kweli, kwa sababu Mungu alisema hivyo. Hilo linalifanya kuwa sahihi, sasa.

Nao walikuwa wakimhukumu Yeye sasa kwa Neno.

41 Sasa kuona kama Yeye alikuwa ni Masihi, ungeweza kurejea kwa yule mtu aliyewapa torati. Mungu aliwapa, hakika, bali Musa aliileta kutoka mlimani, kutoka kwa Mungu. Ndipo akawaambia kwamba angewaacha siku moja. Lakini, "Bwana Mungu angeinua Nabii kama yeye, mithili yake: mtoa sheria, Na—Nabii-Mfalme. Basi—basi itakuwa kwamba kila mtu aliyekataa kumsikia Nabii huyu ataondolewa kutoka miongoni mwa watu." Sasa, waliona hilo, wakati Yesu alipokuja.

42 Na kote katika Maandiko, walikuwa na amri, Wayahudi walikuwa nayo, kwamba, "Akiwepo mmoja miongoni mwenu aliye wa kiroho ama nabii, Mimi, Bwana, nitajitambulisha Mwenyewe kwake katika maono. Na yale asemayo yakitimia, basi msikieni nabii huyo, kwa kuwa niko pamoja naye. Lakini yasipotimia, basi msimsikie." Sasa, hilo ni la busara tu. Hilo ni la kiakili.

43 Kama vile kulivyokuwako na mtu aliyesimama wakati mmoja, Yeremia, nabii mkuu. Bwana alimwambia kwamba—kwamba Yuda ilikuwa inaenda kuwa huko chini Babeli kwa muda wa miaka sabini. Kasema, "Kamwe usimsikilize mwotaji, nabii, wala chochote kisemacho kinyume cha hilo. Akafunga nira shingoni mwake."

44 Ndipo Hanania, sasa, Hanania alikuwa ni nabii. Isitoshe, bali alikuwa ni mwana wa nabii. Baba yake alikuwa ni nabii. Naye akajitokeza, chini ya uvuvio, akaing'oa ile nira shingoni mwake na kuivunja, akasema, "BWANA ASEMA HIVI, katika miaka miwili wanarudi." Watu wangeweza kupiga makofi juu

ya hilo. Jamani, hilo lilikuwa ni zuri! Walitaka kumsikiliza Hanania, bali ilikuwa ni kinyume na Neno. Haikulingana na Neno. Mnaona?

45 Kwa hiyo, Yeremia, yeye alisema, "Hanania, amina, Bwana na ayajalie maneno yako kutimia. Lakini, ngoja kidogo, hebu tukumbuke kumekuwako na manabii kabla ya sisi. Na wakati nabii anapotabiri, naye anajulikana . . . Nabii anajulikana hapo unabii wake unapotimia."

46 Ninawaona marafiki fulani Wahindi wameketi hapa. Nilikuwa nikisoma historia yao, siku moja, katika siku za Wakristo wa mwanzoni za Wahindi. Iliwabidi kufuata mawindo, wapate kuishi. Basi palipotokea nabii miongoni mwao, naye akatabiri na kuwaambia mahali windo lilipokuwa, alifanywa chifu. Lakini kama alitabiri uongo, huo ulikuwa ndio mwisho wa safari yake. Walimwondosha, sasa hivi. Hakuishi tena.

47 Vema, huo ndio msingi ule ule ambao Mungu alitumia. Mungu alimwambia Yeremia, "Hanania amesema uongo. Kamwe sikumwambia hilo." Mnaona, ni kinyume na Neno lake. "Basi ataondoka duniani katika mwaka mmoja." Katika mwezi wa saba yeye akafa. Akamwondosha duniani. Sasa, mnaona, ingawa alikuwa amevuviwa, bali ilikuwa ni kinyume na Neno.

48 Haidhuru mhubiri anaweza kuhubiri kwa nguvu jinsi gani, jinsi anavyoweza kulifanya lionekane zuri, ikiwa ni kinyume na Neno, liondokee. Kaa mbali nalo, kabisa.

49 Ni Neno. Hiyo ndiyo ratiba ya Mungu, ufunuo mkamilifu wa kile Yeye alichokuwa, kile alicho, na kile atakachokuwa. Ni ufunuo unaoendelea wa Yesu Kristo. Na ufunuo mkamilifu wa Yesu Kristo, ni Biblia hii. Lolote linalofunuliwa kinyume na Yeye, kusema yale Yeye angefanya, kile alicho sasa, "Loo, hilo lilikuwa ni katika siku zilizopita," kamwe usiliamini. Haina budi kuwa ni Yesu yule yule, mnaona, na hilo ni Neno, sasa.

50 Sasa tunaona ya kwamba wanafunzi hawa huenda walikizungumzia kisa hicho. Huenda labda Petro alisema, "Mwajua, nilikuwa nikiwazia, mimi mwenyewe, kwamba ninakumbuka baba yangu akiniambia kwamba kutatokea vurugu kubwa siku moja. Daima wamekuwa na mikurupuko midogo. Kwamba kungekuwako, kabla ya kuja kwa Masihi, huenda watatokea masihi wa uongo. Lakini aliniambia, 'Mwanangu, kumbuka jambo hili moja. Sisi ni Wayahudi. Tumechaguliwa na Mungu. Nasi tuna amri kutoka kwa Baba yetu wa Mbinguni, kwamba, na tunajua ya kwamba Masihi huyo atakuwa ni Nabii. Basi ikiwa nabii anajulikana tu wakati anaponena, na yale asemayo yanatimia, kwa hiyo atajua basi kwamba huyo ni Masihi.'"

51 Basi Petro alipoenda Mbele Zake, kwa mwaliko, labda, wa Andrea, ndugu yake, ambaye alikuwa amemsikia, na kuona ile siku ambayo Yohana alimtangaza, na huyo alikuwa Ndiye.

52 Naye Yohana, yeye alimwona Roho, akasikia Sauti. Hakuna mwingine aliyeisikia Hiyo wala kuiona, ni yeye tu. Hao maelfu wote waliosimama pale, hakuna mtu aliyeiona ila Yohana. Ilitumwa kwa ajili yake. "Yohana alishuhudia, akimwona Roho wa Mungu akishuka, mnaona, na Sauti kutoka Mbinguni."

53 Wakati Paulo alipoangushwa na Nuru iliyompofusha, hakuna yeyote wa hao wengine aliyeiona hiyo Nuru. Ilikuwa ni halisi sana, kwa Paulo, hata ikayapofusha macho yake.

54 Wale mamajusi waliifuata ile Nyota kutoka Babeli, kote kote chini. Nao walilinda wakati, kwa nyota. Ikapitia juu ya kila mnara wa kuchunguzia, wala hakuna hata mmoja aliyeiona. Ilionyeshwa kwa mamajusi.

55 Mungu huchagua yule Yeye atakayemchagua, hufanya yale anayotaka kufanya. Yeye ni Mungu. Na Yeye kamwe hataenda kinyume na Neno Lake. Daima pamoja na Neno Lake, sasa.

56 Naye Simoni huenda alisema hivi, mwajua, wakati alipokuwa akinguruma . . . akivuta makasia kuvuka . . . ziwa hili, na Yeye amelala nyuma ya kile chombo. Akasema, "Nilipoenda Mbele Zake, na Yeye akaniambia, 'Jina lako ni Simoni, nawe ni mwana wa Yona,' hilo lilitosha, kwangu mimi. Nilijua basi ya kwamba huyo alikukwa kweli ndiye Masihi, kwa sababu Yeye aliniambia ukweli kabisa, pasipo kuniona."

57 Filipo angaliweza kuwa na ushuhuda wa kumpata Nathanaeli, na Yeye akamwambia mahali alipokuwa kabla hajaja. Wangaliweza kuzungumza juu ya yule mwanamke kisimani. Wangaliweza kuzungumza juu ya Bartimayo kipofu, aliyegusa vazi Lake kwa kusimama yadi mia moja kutoka Kwake, labda, nayo imani ya—yake katika Mungu ikamgusa. Mwanamke aliyegusa upindo wa vazi Lake! Mambo haya yote yalithibitisha kwamba Yeye alikuwa ni Masihi. Ni wakati mkuu jinsi gani!

58 Sasa, basi, huenda walijadijiana juu ya msimamo wa watu kumhusu Yeye. Sasa sisi . . . Wanavuka ziwa, wakati wote. Kuelekea Kwake, wengine walisema, "Wengine waliamini. Wengine hawakuamini."

59 Hivyo ni kama ilivyo leo hii. Watu wengine wanaliamini. La, ungeweza, haijalishi ingethibitishwa dhahiri jinsi gani, wengine hawataliamini. Kisha kuna wengine wao walio wa kiroho sana, hata, ishara ndogo tu ya kwanza, wanalipata. Na wengine wanaweza kushindiliwa, usiku na mchana, nao kamwe hawalipati.

60 Hebu nisimame kwa dakika moja, juu ya hii, na nieleze jambo fulani. Mbegu zinazoanguka ardhini, kama zimerutubishwa, hukua wakati jua linapoziangazia, hali ya unyevu. Lakini kama hazijarutubishwa, jua linaweza kuziangazia, zitaoza tu, vivyo hivyo. Hakuna kitu kitakachotukia.

61 Tumerutubishwa. Majina yetu yameitwa, yakawekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwanakondoo, kabla ya kuwekwa msingi wa ulimwengu. Haijalishi sisi ni wa kidini jinsi gani, hilo halina uhusiano wowote nalo; wakati mwingine linatupinga.

62 Ninajisikia nyumbani na ndugu mzuri sana kama Ndugu Groomer hapa, na ndugu hawa wengine hapa. Na—najisikia tu kusema jambo hili.

63 Mtazameni Yesu. Tunajua sasa Yeye alikuwa ni Masihi. Na wakati alipokuja na kujionyesha Mwenyewe Masihi, juu ya watu wa kidini, Mafarisayo, Masadukayo, wote kutoka kwa makuhani waliotoka kwenye ukoo wa Haruni, kwa mamia mara mamia ya miaka. Baba wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu wa babu zao huko nyuma kabisa, mababu, walikuwa ni makuhani, wakilisoma Neno, wakiwasoma manabii. Nao manabii walinena dhahiri juu ya hili. Lakini wakati Yesu alipokuja na kutenda hilo, walikuwa ni vipofu kama popo. Wa kidini kwelikweli, werevu, wenye akili, wenye elimu wawezavyo kuwa, mbali zaidi ya yeyote miongoni mwetu siku hizi, wamefunzwa katika Neno, walilelewa tangu utotoni. Ndipo wakati ile Kweli halisi ilipoangaza kote mbele zao, nayo hiyo Nuru ikamulika, wao walisema, "Mtu huyu, hatuwezi kuelewa hilo, kwa hiyo hana budi kuwa ni ibilisi, Beelizebuli. Yeye ni mtu mwenye akili nyingi sana. Anaweza kusoma akili za watu." Mwanatelepathia, tungeweza kumwita leo hii. Hawakuelewa.

64 Lakini sasa angalieni. Siku moja, huko Sikari, mji mdogo wa Samaria, basi Yesu akapitia pale akaketi kando ya ukuta. Basi maskini mwanamke mmoja, mwenye sifa mbaya, jina baya; alikuwa na waume wengi asiopaswa kuwa nao. Naye huyu hapa anakuja, kuchota maji. Ndipo Yesu akamwambia, "Nipe maji ninywe. Na niletee maji ninywe." Ndipo akamwambia ya kwamba wa—wasingeweza kufanya hivyo. Haikuwa sahihi. Ilikuwa ni matusi kwake kuninii. . .Kwake kumwomba mwanamke Msamaria kitu kama hicho.

65 Ndipo akamwambia upesi, "Kama ungalijua ni Nani uliyekuwa ukisema naye!" Sasa, yeye hakujua. Kasema, "Kama ungalijua ni Nani aliyekuwa akisema na wewe, ungeniomba Mimi maji unywe."

66 Hoja hiyo ikaendelea kwa kitambo. Baada ya muda mfupi, Yesu, akiwa ametumwa pale kisimani, alimwambia, "Nenda, kamwite mume wako."

67 Akasema, "Sina yeyote." Angali alikuwa amepofushwa, mnaona, kwa sababu mtu yeyote angeweza kufundisha theolojia, mnaona, ama anaweza kutoa tamshi la namna yoyote. Anaweza kusema lolote atakalo, hilo bado halilifanyi kuwa sahihi.

Akasema, "Nenda, kamwite mume wako."

Akasema, “Sina mume yeyote.”

68 Yeye akasema, “Umesema kweli, kwa kuwa umekuwa na watano, na yule unayeishi naye sasa siye wako. Umesema kweli.”

69 Angalia Nuru hiyo ikigusa chembe ile ya Uzima. Huo mmea ukaanza kukua. Upesi, kiajabu, upesi; kahaba huyu, aliyeteseka sana, aliyetupwa nje, sio kasisi aliyefunzwa! Mwanamke katika maisha mabaya, bali alikuwa amekusudiwa Uzima wa Milele tangu zamani. Basi wakati Nuru hiyo ilipoigusa, upesi akaitambua.

70 Akasema, “Bwana, naona kwamba Wewe ni nabii. Sasa, hatujawa na mmoja kwa miaka mia nne, bali hata hivyo tunajua kwamba Masihi yuaja. Naye Masihi huyo atakuwa ni nabii, na Yeye atatwambia mambo haya.” Mnaona, yeye alijua Mtu ambaye alimwambia hayo asingemwambia uongo.

71 Na Yeye alijua hilo. Ndipo akasema, “Mimi Ndimi, ninayezungumza nawe.”

72 Hakuuliza swali lingine, lakini, akaingia mjini, na kusema, “Njoni, mwone Mtu!”

73 Angalieni tofauti. Mnaona, wakati Nuru hiyo inapopiga, ama itapofusha ama kufanya Hai. Mnaona? Haina budi. Uzima, Andiko la Biblia!

74 Sasa, huenda kulikuwa na mambo mengi ambayo watu wangalizungumzia. Baadhi yao walisema hivi, “Hajanena kamwe mtu yeyote kama Mtu huyu.” Baadhi yao waliamini, kasema, “Mtu huyu anaonekana kuwa na mamlaka. Anaonekana kuwa na hakika kabisa katika yale anayozungumzia. Kamwe hatujaona mtu ambaye angeweza kusimama na kusema tu mambo namna hiyo. Tumewasikia makuhani wakizungumza. Tumewasikia marabi, makuhani, na wote, kila kitu, na mihadhara, na kadhalika. Lakini Mtu huyu anazungumza kwa mamlaka. Anajua yale anayozungumzia. Kamwe mtu hajanena namna hiyo.”

Wengine wakasema, “Yeye ni Beelizebuli.”

75 Hapana shaka ilikuwa ni Yohana, jamaa mdogo, mwajua, akiwaza haraka. Hapana shaka ilikuwa ni yeye aliyesema, “Liwazieni tu! Yule ambaye angezichukua biskuti tano na samaki wawili, na kuwalisha elfu tano, amina; Yule ambaye anajua siri za moyo; Yeye yuko pamoja nasi, chomboni. Tunaye papa hapa. Ndugu, mnashuhudia,” huenda alisema, “lakini Yule tunayemwazia, Yeye yupo papa hapa pamoja nasi.”

76 Hilo ni jambo lile lile sasa hivi, Yule tunayehubiri habari zake, Yule tunayezungumza habari zake. Mungu wa Musa anafaa nini kama siye Mungu yule yule leo? Yule tunayenena habari zake yupo hapa pamoja nasi. Loo, ni jambo la jinsi gani kuwazia!

77 Halafu basi, mnaona, pia walikuwa kwenye ziwa lenye hatari. Na ni hi—hisi ya jinsi gani ya usalama, wakati wakiabiri

kwenye zi—ziwa lililojaa tufani, kujua ya kwamba Huyo alikuwa amelala pamoja nao, chomboni.

78 Jinsi unavyoweza kuwa salama! Wakati bahari zimechafuka, wakati hazijachafuka, kamwe haileti tofauti hata kidogo. Mradi tu unajua Yeye amekaa papo hapo, inaleta tofauti gani? Yaje, yaende, chochote kile, haileti tofauti hata kidogo. Liko hapo. Ninalijua. Unasema, "Mimi...Abarikiwe Bwana!" Daktari aseme utakufa kwa kansa; sema tu, "Utukufu kwa Mungu! Safari ya haraka ya kwenda Nyumbani, labda." Mnaona? Hawajali.

79 Nikizugumza, na kundi la madaktari, hivi majuzi. Yeye alisema—alisema, "Nilisoma kitabu chako juu ya uponyaji wa Kiungu."

Nikasema, "Nadhani ulikosoa."

Kasema, "La, bwana. Ninakubali kwamba unasema kweli."

Nikasema, "Asante, Dk. Schoen."

80 Yeye akasema—akasema, "Ndugu Branham, tuna kumbukumbu kwamba tunapomwambia mtu aliye na ugonjwa wa kufisha, ama—ama kitu ambacho kinaenda kumwua, kidonda kilicho tayari kupasuka, ama kifua kikuu, inategemea msimamo wanaochukua. Kama wakivurugika kabisa," kasema, "wanakufa mara moja. Lakini," kasema, "kama wakichukua msimamo, 'Vema, kufa ni sehemu tu ya kuishi. Ni sawa, nitakapokufa,'" kasema, "unajua, karibu inaudumaza ugonjwa huo?"

81 Nikawazia tu, "Kama msimamo huo wa kiakili, ukichukuliwa namna hiyo, utafanya nini wakati Roho Mtakatifu anapomgusa huyo mtu wa ndani?" Hilo hapo. Ni...Nilimwuliza hilo.

82 Akasema, "Hakika, hiyo ni kweli, kama unaweza kuingia mahali fulani, uingie katika hilo." Mmoja wa wapasuaji hodari na madaktari aliyeko katika eneo la kusini, alisema, "Kama ni...Bw. Branham, inaweza kuthibitishwa. Kama mtu atasogea, anaweza kusogea aingie mahali hapo, mpaka hata akili yake mwenyewe hata haijui anao, kuwazia anao, na hata asiuzingatie," kasema, "ingetendeka, ikiwa anaweza kuamini hilo." Hiyo ni kweli. Mnaona?

83 Msimamo wa kiakili unaochukua kuuhusu utasababisha... Sasa, nia haitafanya hivyo. Lakini kama ukichukua msimamo huo kwa kitu kilicho na Uzima ndani yake, basi Uzima huo hushuka na kufanya hilo. Sio msimamo wako wa kiakili; huo unakuleta tu katika Uwepo Wake. Hivyo ndivyo unavyofanya, nia yako. Zile hisi tano ni sawa mradi hazimkani Mungu. Lakini zinapoanza kumkana Mungu, basi achana nazo. Mungu huzitawala. Huyo ni Muumba.

84 Sasa, ni usalama wa jinsi gani, kama nilivyosema, wakisafiri kwenye bahari hii iliyochafuka, wakijua ya kwamba Yeye amelala mumo humo ndani ya chombo. Kuna kitu hao wanafunzi walichokuwa usiku huo, kama tulivyo usiku wa leo, walikuwa wakifurahia matokeo ya mkutano; baada ya uamsho, wakiyafurahia matokeo ya huo uamsho.

85 Sasa, Ndugu Groomer, na ndugu hapa, na wengine wengi. Yapata miaka kumi na mitano iliyopita tulipitia humu nchini, na kulikuwako na uamsho. Jamani! Nanyi mnajua yale tunayofanya leo hii? Tunazungumza tu juu yake. Uamsho umekwisha. Umekuwa umekwisha, muda mrefu. Tunaishi tu kwenye matokeo yake, tukingojea.

86 Nao hao wanafunzi walikuwa wakifanya jambo lile lile, wakishangilia, wakiishi juu ya yale waliyokuwa wameona yakifanywa, labda siku iliyotangulia, na juma lililotangulia, na mwaka uliotangulia. Walikuwa wakishuhudia juu yake, wakitoa, loo, ushuhuda mkuu wake.

87 Tunajuaje kwamba, kama vile Yesu katika siku yao alikuwa akipumzika katikati ya miamsho, tunajuaje labda Yeye anapumzika sasa katikati ya miamsho? Naam.

88 "Loo," mnasema, "sasa, ngoja kidogo, Ndugu Branham; unaenda kando kidogo ya njia sasa. Yesu hana haja ya kupumzika."

89 Naam, Yeye alipumzika. Biblia ilisema hivyo, "Mungu aliumba mbingu na nchi katika siku sita, na ya saba Yeye akapumzika." Hakika alifanya hivyo. Alipumzika. Yesu, akiwa amechoka, amelala kwenye chombo, alikuwa amelala usingizi na anapumzika.

90 Na labda baada ya kazi ngumu ya ule uamsho ambao ndio kwanza upite, labda Yeye anapumzika sasa kama alivyofanya wakati huo. Natumaini ndivyo.

91 Nao wanafunzi walikuwa wakishangilia juu ya yale waliyokuwa wamemwona akifanya, mnaona, huku wakijua kwamba Yeye alikuwa pamoja nao.

92 Hiyo kidogo ni kama mwanadamu, akili ya mwanadamu. Akili ya mwanadamu sikuzote inanena na kushangilia yale Mungu amefanya, nao wanasema yale atakayofanya, na kupuuza yale anayofanya.

93 Hakuwa amelala, hasa. Tutalifikia hilo, katika dakika chache. Mnaona?

94 Wataamini yale amefanya, na kupaza sauti kuyahusu. Watanena juu ya yale atakayofanya, na kumtukuza Mungu. Bali yale anayofanya sasa hivi, wanayapuuza. Hiyo ni tabia tu ya mwanadamu. Hivyo ndivyo tu yeye afanyavyo.

95 Halafu, wakati walipokuwa wakizifurahia baraka za ushirika wao, mmoja kwa mwingine, ndipo, loo, wakiyahesabu

yote, yale waliyokuwa wameona yakifanywa, mara ghafla shida ikaibuka.

96 Na hiyo ni kama tu Shetani, kufanya hivyo, mnaona, papo hapo wakati mnapokuwa na mkutano wa ushuhuda ama kitu fulani. Mara nyingi mimi . . .

97 Hapa si muda mrefu uliopita, nilikuwa kwenye mkutano, nikijiandaa tu kufanya wito wa madhabahuni. Ndipo maskini jamaa mzee akaanguka ghafla moja kwa moja sakafuni, mfu awezavyo kuwa, mnaona, katika mshtuko wa moyo. Na mahali hapo pote pakavurugika. Nami ninasahau . . . Ilikuwa huko Shawano, Wisconsin. Nikawaza, "Mungu, nifanye nini?" Nikaangalia *hapa*, nami nikamwona mzee huyo katika ono, akitoka mlangoni. Ninajua la kufanya wakati huo.

98 Si muda mrefu uliopita, pamoja na mdhamini huyu mkubwa wa Oral Roberts, daktari huko juu Philadelphia, ni nini hicho? Yeye ni . . . Ninasahau jina lake sasa. Yeye ni daktari wa meno. Ni mdhamini mkubwa wa kipindi chake cha televisheni. Siwezi kulikumbuka jina lake. Nasi . . . [Mtu fulani anasema, "Barton."—Mh.] Barton. Tulikuwa na mkutano, nami nilikuwa tu ninajiandaa kufanya wito wa madhabahuni. Ndipo nikamwona mwanamke akitenda katika hali ya kushangaza sana, ndipo binti yake akakimbia pale, akaanza kupangusa uso wake. Nikawaza, "Vema, yeye huzirai mara kwa mara." Ndipo ghafla, miguu yake ikanyoka mara moja, na mikono yake ikarudi nyuma namna *hii*.

99 Dk. Barton akakimbia mahali alipokuwa, akapima mapigo yake. Hakuwa na yoyote. Akaniangalia, akakitikisa kichwa chake. Vema, nikajaribu kuziweka nia za watu . . . Walikuwa wameketi huko nje, umati mkubwa. Nikaliacha, namna hiyo, nikaendelea tu, kuzungumza. Na kwa hiyo yeye akasema, "Nendeni mkamlete Branham mdogo." Huyo ni Billy. Ndipo Billy akamwona mwanamke huyo aliyekufa. Hakuwa na chochote cha kufanya na hilo. Mnaona? Hakutaka hilo. Vema, mara tu nilipoanza kuzungumza tena . . . Sasa, Dk. Barton, kwa kuwa mnamfahamu, mnaweza mkamwuliza.

100 Nilipoanza kunena tena, nikasema, "Sasa, kila mmoja, msitaharuki. Nyamazeni." Wakati mwingine unapomwona pepo akijaribu kumtoka mtu, wanakuwa wasio na kicho sana, umati unavurugika. Hilo ni jambo baya la kufanya. "Ketini kimya. Msitaharuki. Yeye yupo hapa."

101 Ndipo nilipokuwa nikizungumza namna hiyo, sijui jinsi lilivyotukia, lakini nilimgeukia na kuliita jina lake. "Mary, angalia hapa." Basi alipofanya hivyo, akajirudia, akajirudia.

102 Mnaona, ni wakati huo wa shida. Mara tatizo linaibuka, wakati ufaao kabisa.

103 Sasa, sasa, huenda mkamwuliza Dk. Barton kuhusu hilo. Nilikutana naye kesho yake, naye akasema, "Ndugu Branham,"

kasema, "mwanamke huyo hakuwa na moyo. Nilimchunguza hapa chini tu—tumboni mwake. Nikauchunguza moyo wake shingoni mwake, kila mahali." Kasema, "Alikuwa ameaga." Halafu, basi, walikuwa ni familia tajiri sana, na ilikuwa ndiyo mara ya kwanza aliyowahi kuwa katika mkutano kama huo. Ndipo yeye . . .

104 Nikaenda, akanipeleka nyumbani mwake, naye akasema, "Nilikusikia ukiliita jina langu." Na mimi sikuwa nimewahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu, bali ilikuwa ni Roho Mtakatifu. Mnaona?

105 Sasa, mara ghafla, shida ikainuka. Meli ikaanza kuyumba. Mawimbi yakapanda juu. Nayo, matanga, labda upepo ulishuka tu kwa mvumo wa hasira na kuipiga moja kwa moja kutoka kwenye nguzo ya mlingoti. Ndipo hiyo meli ikayumbayumba sana, nayo yale mawimbi makuu yakawa meupe na kurusha maji humo chomboni. Na chombo kikaanza kujaa maji. Tatizo! Matumaini yote ya kunusurika yalionekana kutoweka, ingawa walikuwa wamemwona akifanya mambo mengi sana. Walikuwa wameyaona, lakini, shida ilipoingia, yote yakasahaulika.

106 Nashangaa kama hivyo sivyo tu ilivyo usiku wa leo. Tunajua yale tumemwona Mungu akifanya katika uamsho huu. Ninyi wahudumu mnajua hilo. Mnaona ngu—nguvu Zake. Ninii Yake, jinsi alivyowafufua wafu; taarifa ya daktari. Alitabiri mambo yaliyotukia, juu ya alama. Amewaponya wagonjwa. Maelfu mara maelfu wameponywa, kote ulimwenguni. Lakini sasa wakati kile kipindi kidogo cha utulivu kinapokuja, ndipo basi wakati matatizo yanapoingia, sisi tunasahau upesi hivyo?

107 Ni kama tu Israeli, Yeye akiisha kuleta mapigo yote huko Misri, na kutenda mambo makuu aliyotenda. Ndipo walipofika kwenye Bahari ya Shamu, ilimbidi Musa kusema kwa sauti kuu, "Mmeona miujiza kumi, na bado mnamtilia shaka Mungu?" Wakati hawakupata maji kwenye shimo la kale la kunywea, walikuwa wakinung'unika, wakiteta. Hao ni wanadamu tu. Walisahau miujiza yote aliyofanya. Mnaona? Tunasahau, pia.

108 Labda wanafunzi hawa walikuwa wameyapata yote, maana ni wakati wa shida. Sasa wakati tunapopata ninii . . . Walikuwa wameingia katika shida ambayo wasingeweza kupata suluhisho lolote kwa ajili yake. Mradi tu tunaweza kupata suluhisho, tunalishikilia moja kwa moja. Lakini walikuwa wameingia katika tatizo ambalo wasingeweza kupata suluhisho, ndipo wakaogopa. Wakalia. Waliogopa wakati hawakuwa na suluhisho.

109 Nilijiahidi nitaliachilia kanisa litoke hapa saa tatu. Kwa hiyo ningeweza kudumu kwenye hilo muda mrefu, bali ni—ninajaribu tu kugusia sehemu muhimu, ambapo mnaweza kuona.

110 Ndugu, kuna shida nyingi usiku wa leo ambazo hatuna suluhisho kwa ajili yake. Ninao mlolongo, orodha hapa

chini, matatizo ya kitaifa. Hawawezi kutatua suluhisho lolote. Hawajui jinsi ya kulifanya. U.N., Mashirikisho ya Mataifa, na mazungumzo haya yote, yanazidi kuzorota wakati wote.

111 Usiku ule huko Ufini, wakati yule mvulana mdogo alipokuwa ameuawa barabarani siku hiyo. Meya wa mji ameliandika, nami ninayo imetiwa sahihi kwa muhuri wake. Niliona ono lake, miaka kadhaa hapo kabla. Wakati nilipopitia Arizona hapa, nikiwaambieni juu yake, "Kutakuwako na mvulana mdogo atakayefufuliwa katika wafu, na sura yake." Nyote mnalikumbuka, wengi wenu. Sasa, lilitukia vivyo hivyo tu. Niliwaambia lingetokea katika *Sauti Ya Uponyaji*. Likatokea, yapata miaka miwili baadaye, ama mitatu. Mnaona? Sasa, wote wamesumbuka, na huko kupiga kote makelele, na kulikuwa na tiba. Mungu alikuwa na tiba, na Yeye akamponya mvulana huyo mdogo.

112 Usiku huo, nikiteremka barabarani huko Kuopio. Basi tulipokuwa tukishuka mtaani, yapata sita wa maskini wavulana hawa wa Kifini. . . Walikuwa tu wamemaliza vita hivyo, na maskini jamaa hao hawakuwa wamenyolewa. Ilikuwa—ilikuwa . . . Walikuwa ni wavulana wadogo iliyowabidi kuwaingiza katika jeshi. Hao Warusi wakawaua. Nao walikuwa wakishuka kwenda kule, wakiwa na visu hivi vikubwa, virefu, vya kale vyenye meno, wakizuilia umati, wakati nikishuka kwenda kwenye kile walichokiita Messuhalli, ambapo waliwaruhusu yapata elfu thelathini na tano, kisha wanawaacha watoke, kisha wananiacha niwazungumzie wengine elfu thelathini na tano ama arobaini.

113 Na kote barabarani, walisimama askari wa Kirusi. Ndipo nilipopitia hapo, pamoja na saluti ya Kirusi, na machozi yakitiririka mashavuni mwao. Ndipo nilipopita hapo, waliwanyakua hao askari wa Kifini na kuwakumbatia. Ndugu, chochote kitakachomfanya Mrusi amkumbatie Mfini, ama Mfini kumkumbatia Mrusi, kitamaliza vita. Wamepitia juu ya kitu kinachomaliza vita, bali kamwe hawataweza kupata tiba kwa mafanikio ya kubuniwa na wanadamu.

Tayari imetayarishwa. Mtu mmoja alikufa kwa kusudi hilo.

114 Kanisa lina matatizo ambayo hawana suluhisho lolote kwa ajili yake. Wamethodisti wote watawezaje kuwafanya Wabaptisti wote kuwa Methodisti? Ninashangaa tu. Waassemblies wote watawafanyaje wa Umoja wote kuwa Assemblies, ama Waassemblies waende vinginevyo? Wapentekote wote watawashawishije Wapresbiteri wote, Walutheri? Nayo Katoliki itachukuliaje kitu hicho chote? Mnaona? Kamwe hawawezi kulielewa, ni nani kati yao atakayetawala. Mnaona? Hawajui. Hawana tiba. Vema.

115 Lakini, hivi mlijua, wao hawakuwa na tiba jinsi ya kuikomesha ile dhoruba, bali tiba ilikuwa imelala pale.

116 Basi hebu niseme hili, ndugu, usiku wa leo. Katika matatizo yetu yote, tungali tunayo Tiba. *Hii* hapa, kwa kuwa Yeye ni Neno. Limewekwa papa *Hapa*, naye Roho Wake yuko papa hapa kulidhihirisha. Kwa hiyo, tunayo Tiba. Lakini tunajaribu kupata mambo mengine, kuanzisha dhehebu lingine. Hao ni sisi. Mnaona? Hatuwezi kulidhibiti. Tayari limedhibitiwa. Tunashindwa tu kutembea katika njia iliyodhibitiwa kwa ajili yetu.

Lakini walifadhaika.

117 "Ikiwa watafanya ibada ya uponyaji kule chini kwa Groomer, vema, unajua kuna jambo fulani kuwahusu hao watu ambalo silipendi. Wao ni watakatifu wanaojibingirisha. Siendi huko chini." Vema, haya basi. Mnaona? Jambo ndilo hilo. Hivyo ndivyo tu ilivyo. Mnaona? Naam. Ni. . .

118 Bali Kristo ndiye Tiba hiyo. Yeye ndiye kitu kinachoweza kufaulu. Wanafunzi Wake, leo hii, wanaingia katika matatizo mengi sana, nao hawaijui Tiba. Hiyo ni kweli.

119 Basi hebu niseme hili. Mara nyingi watakatifu Wake wa thamani huingia katika shida, pia, matatizo ya kimwili, bali hapa tunayo Tiba. Amina. Tunayo tiba.

120 Ninawazia juu ya mwanamke huyu aliyeketi hapa akiwa na ugonjwa wa pafu, basi; oksijeni hii, namsikia akipumua ndani yake. Ninawazia jinsi maskini huyo hulala usiku. Wazia matumizi yaliyopo. Dada, pale, mimi ninajua Tiba. Ipo *Hapa*. Haikulazimu kufanya hivyo. Lakini huna budi kuitumia Hiyo. Unaona?

121 Sasa, wale wanafunzi waliingia katika matatizo ya kimwili, matatizo ambayo madaktari hawana tiba.

122 Kama tu wale wanafunzi, walikuwa na matatizo. Walikuwa ni wanafunzi, nao walikuwa—walikuwa na shida ambayo mabaharia wasingeweza kutatua. Wao. . .Hakuna mtu angaliweza kuyatatua, bali Tiba ilikuwa imelala pale pale.

123 Nawe huenda ukawa na tatizo usiku wa leo ambalo daktari hawezi kutatua. Lakini tunaye papa hapa sasa, kama walivyokuwa naye. Yeye yupo papa hapa. Hiyo ni kweli. Sisi, kama wale watu, tulisahau Huyu ni nani aliye kwenye chombo. Si tu kanisa. Si tu kanuni tunazofuata. Bali ni Muumba wa mbingu na nchi. Huenda anapumzika sasa hivi kutoka kwa uamsho. Alimtuma mmoja. Huenda anapumzika.

124 Alikuwa na mwingine mbele Yake, kesho yake, mwendawazimu ilibidi aponywe. Lakini, wakati huo, Yeye alikuwa akipumzika, ndipo tatizo likaingia. Na Yeye alikuwa amelala, akipumzika. Lakini wao walisahau Huyo alikuwa ni Nani, mnaona, katika ghasia hizo. "Vema, ninajua, lakini vuta *hilo* kasia, Simoni. Andrea, kwa nguvu zaidi *hilo* kasia! Tutafanya nini?" Mnaona? Hilo hapo.

125 Umechanganyikiwa sana hivi kwa nini? "Daktari alisema *hili*. Daktari alisema *lile*." Vema, labda alisema. Labda mtu huyo yuko sahihi. Hilo ndilo alilosema. Lakini, Hili linasema nini? Hilo ndilo jambo linalofuata. Mnaona?

126 Na jambo lingine. Baada ya wao kumjua jinsi walivyomjua, iliwapasa kujua ya kwamba Mtu ambaye angeweza kuyatambua mawazo ambayo mtu mwingine alikuwa akiwazia, na alijua mwisho tangu mwanzo, alijua litatukia kwa vyovyote vile. Amina. Sasa, usikose, usikose hili. Yeye alijua lilikuwa linaenda kutukia. Ninatilia shaka sana kwamba alikuwa amelala. Bali alijua lilikuwa linaenda kutukia. Yeye alikuwa ni Mungu, naye Mungu hana kikomo, kwa hiyo Yeye alijua litatukia. Pia alijua wakati lilikuwa linaenda kutukia. Nalo lilitukia tu, kuijaribu imani yao. Hivi Yeye hakusema hivyo, baadaye?

127 Na hiyo ndiyo sababu u mgonjwa usiku wa leo, labda. Hiyo ndiyo sababu kipindi cha utulivu wa uamsho kimeingia, aone utakalofanya juu ya yale umeona yakifanywa. Utayaokota, ukaunde dhehebu lingine kutoka kwake?

128 Mungu yule aliyejitokeza jukwaani, wakati dada huyu, anayeketi hapa, walipomleta mstarini, hapa chini kwenye lile kanisa dogo la Kimeksiko siku hiyo, kansa moyoni. Daktari wake anayo eksi-rei. Mume wake ameketi pale. Wao walisema, "Yupo mwanamke aliyekufa mstarini."

Nikasema, "Mlete huku." Nilikuwa na hakika kwamba Yeye alikuwapo.

129 Dada Waldrop, huo umekuwa ni muda mrefu uliopita, miaka kumi na sita. Mnaona? Akifa, kwa kansa! Kumbukeni, Mungu yuyo huyo angali kwenye meli. Msichanganyikiwe. Huo hapo ushuhuda ambao ungeweza kuipindua Phoenix, hili Bonde la Maricopa, ama ulimwengu, juu chini, mmoja kutoka makumi ya maelfu.

130 Angali hapa. Bali tunachanganyikiwa kabisa, mnaona, kama walivyofanya. "Loo, jamani! Vuta kasia *hili*. Tutafanya nini tena?" Sasa, usiwazie hilo. Mradi tu Yeye yuko ndani ya chombo, lisahau. Bila shaka. Sasa, Yeye alifanya hivyo tu apate kuijaribu imani yao. Na hivi Maandiko yetu hayatwambii ya kwamba, "Majaribu haya yamewekwa juu yetu, na ni ya thamani zaidi kwetu kuliko dhahabu?" Hutufikirii hivyo, bali Biblia ni sahihi.

131 Ungeweza kumuwazia Ayubu akifurahia kushikwa na majipu, na vitu hivi vyote vimeangamia, akipoteza mali yake yote na watoto wake, na kila kitu? Haikuwa ni rahisi sana, bali Mungu alikuwa akimthibitishia Shetani kwamba Yeye alikuwa na mtu fulani angeweza kumtumainia. Labda anajaribu kufanya jambo lilo hilo katika kisa chako, na ninyi wengine. "Loo, watakuacha. Wataninii . . . " Loo, la. Ayubu, wasingeweza kumfanya Ayubu kufanya hilo. La, bwana. Mnaona? Yeye anajaribu tu kuwathibitisha.

132 Kumbukeni, katika dakika chache, Yeye alisema, "Loo, enyi wenye imani haba. Hivi hamngeweza kufahamu kuhusu kuvunja mikate na kuwalisha elfu tano? Hivi hamjui Mimi ni Yehova yeye yule aliyewalisha hao miaka arobaini huko nje nyikani, kutoka kwa matanuru, kutoka Mbinguni, wakati nilipoimwaga kila usiku? Unahofia nini sana hivi? Hivi hamjui niliikausha Bahari ya Shamu, siku moja? Hivi hamjui niliifungua ardhi ikammeza asiyeamini? Siku moja niliipima ardhi na kuirusha, ikaingia huko angani." Na Yeye yuko chomboni. Sasa, hiyo si hadithi ya kubuni. Hiyo ni kweli. Naam.

133 Vivyo hivyo sasa. Yeye hujaribu kututhibitisha aone mahali tutakaposimama, ama sivyo. Anaondoa uamsho, na kuanzisha ubishi kanisani, apate tu kuona kile mtakachofanya. Anamwachilia Shetani miongoni mwenu, miongoni, aone jinsi mtakavyosimama. Anamwacha awapige kwa kitu fulani, aone mtachukua msimamo wa namna gani. Ayubu alisema, "Hata akiniua, bado nitamtumaini." Amina. Amina. Jambo ndilo hilo.

134 Shadraka, Mishaeli, na Abedinego, walisema, "Mungu wetu anaweza kutukomboa na moto huo, bali hata hivyo hatutasalimu amri." Hakika.

135 Lakini tunachanganyikiwa kabisa, mwajua, kama walivyofanya, hao wanafunzi. Wao. . . Sisi ni wanadamu, kama tu hao walivyokuwa.

136 Na Yeye alikuwa amethibitisha kwamba Yeye alikuwa ni nani, na halafu, bado, akiisha kujithibitisha kwamba ni Mungu wa viumbe. Yeye alikuwa ni Muumba. "Alifanyaje hivyo? Vema, hebu niambie ni kitu gani alichofungulia, kupika huo mkate na kupika samaki hao." Vema, Yeye—Yeye hakuumba tu samaki, bali alipika hao samaki, wakati uo huo. Hilo ni kweli.

137 Hiyo mana ilitoka wapi, kutoka Mbinguni, chakula halisi kilichowaweka watu hai miaka arobaini? Mkate, ulishuka kutoka Mbinguni. Yeye aliupata wapi?

138 Wale kunguru walipata wapi nyama hiyo na mkate, kumlisha Eliya? Akili ya kunguru, kupika nyama, na kumchinja ng'ombe na kumkatakata, na kumpika na kufanya mnofu, na kuiweka kwenye mkate na kuuoka, kisha kumletea Eliya.

139 Yeye ni Mungu. Tusipoliamini, basi sisi ni wasioamini. Hivyo tu. Hatuna budi kuamini.

140 Hivyo ndivyo Ibrahimu alivyofanya, "Aliita kila kitu kinyume chake kana kwamba hata hakikutendeka." Haijalishi jinsi alivyozeeka, ama kiasi gani, aliendelea tu kumsifu Mungu kwa ajili ya ile ahadi, akaendelea nayo.

141 Sasa, Yeye alithibitisha kile alichokuwa, kwa Neno Lake na ishara zilizothibitishwa. Alisema, "Kama sizitendi kazi zilizoandikwa kunihusu Mimi, basi msiniamini Mimi." Mnaona? Sasa, hivyo ndivyo unavyolishika. Ninatumaini ya kwamba

mnatafakari kwa kilindi sana hapa. Mnaona? Daima liangalieni Neno hilo.

142 Hilo ndilo—hilo ndilo Shetani alimshambulia Hawa kwalo, katika bustani ya Edeni, na kumwondoa kwake kwa hoja, kwa hoja.

143 Bali aliporudi na kumshambulia Kristo, yeye alimtupia hayo mambo moja kwa moja tena. Alisema, "Kama wewe ni Mwana wa Mungu, sasa ningetaka kuona mwujiza. Wajua, sijawahi kuona mmoja. Ningetaka uyageuze haya . . . Una njaa. Yafanye mawe haya mkate."

144 Yeye akasema, "Imeandikwa . . ." Loo, jamani! Haya basi. Juu ya mnara wa hekalu, "Imeandikwa . . ." Juu ya mlima mrefu, "Imeandikwa . . ." Alidumu moja kwa moja na Neno hilo, na kumweka jamaa huyo wa kale moja kwa moja mahali pake.

145 Sasa, Yeye aliwaambia hao jamaa ambao hawakumwamini, waliodhani Yeye alikuwa ni mpiga ramli ama—ama namna fulani ya Be—Be—Beelizebuli, ibilisi, chini ya kuwasiliana na mizimu, kwamba Yeye aliyajua mawazo ya mioyo ya watu, na kadhalika, akijaribu kufanya hivyo. Alisema, "Ni nani kati yenu anayeweza kunishuhudia Mimi ya kuwa nina dhambi?" Akasema tena, "Msiponiamini Mimi," kasema, "yachunguzeni Maandiko, kwa kuwa ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele; na hayo ndiyo, hayo Ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Ndiyo kitu kinachoifanya huduma Yangu kile ilicho." Mnaona ninalomaanisha? "Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi." Mnaona? Akirejea (kitu gani?) moja kwa moja kwenye Maandiko tena. "Hayo ndiyo yanayonishuhudia Mimi. Yanawaambia kwamba Mimi ni Nani." Amina. Utukufu kwa Mungu!

146 Maandiko yanakuambia kama wewe ni mwaminio ama sivyo. Maandiko yanakwambia kama unaenda sawa ama la. Hivyo ndivyo unavyomfahamu mtu, kwa ushuhuda wake. Si yale asemayo kwa *hiki*, bali jinsi anavyojiweka sawa na Maandiko. Kweli. Hivyo ndivyo mnavyojua hilo.

147 Yesu aliwaalika kufanya hivyo. "Kama sikutimiza kila sifa ya Masihi, basi niambieni mahali nilipokosea." Loo, jamani! Hilo ni jambo zuri. Sivyo? "Niambieni mahali nilipokosea, kama sikutimiza hizo sifa, kama nimetenda yale hasa Maandiko yaliyosema ningefanya."

148 Loo, Mkristo, laiti tungalijilainisha wenyewe mle ndani, tufanye yale Maandiko yanayosema Mkristo apaswa kufanya!

149 Walipaswa kujua Yeye alikuwa ndiye Mungu wa viumbe. Naye angeweza . . . Yeye ndiye hasa aliyeyaumba maji na upepo. Walipaswa wawe wamejua hayo. Na kama walijua ya kwamba Yeye alikuwa hivyo, hivi hawakufahamu ya kwamba kiumbe hiki cha muumba kilipaswa kulitiii Neno Lake, loo, jamani, kama Yeye alikiumba? Ni nani aliye mkuu zaidi, kiumbe ama Muumba? Kama Yesu alivyosema, "Ni nani aliye mkuu zaidi,

yeye aliyetumwa, ama Yeye aliyemtuma?" A-ha. Mnaona? Ni nani aliye mkuu zaidi, kiumbe ama Muumba? Muumba. Nao waliona, na Yeye akathibitisha, ya kwamba Yeye alikuwa ndiye huyo Muumba. Na basi kama Yeye alikuwa ndiye huyo Muumba, angeweza, hivi kiumbe Chake kisingemtii?

150 Hebu tukumbuke pia ya kwamba Yeye aliiumba miili yetu. Hivi miili yetu haitatii amri Yake? "Tema kansa hiyo," Yeye anauambia mwili, na hiyo inaondoka. Wewe lichukue tu hilo Neno na ulipande humu ndani uone kinachotukia. Hakika. Naam, bwana. Miili yetu haina budi kutii amri Yake.

151 Unasema wewe ni Mkristo. Ninaamini ndivyo ulivyo. Unaamini. Unatulia ndani ya nini? Siku moja Yeye ataifufua miili yetu, ikiisha kuangamia kabisa, kwelikweli. Ikiwa huamini hilo, kwa nini uende kanisani? Unaona? "Kama hakuna ufufuo, hivi sisi, miongoni mwa watu, si tuna mashaka zaidi?"

152 Lakini Neno Lake la ahadi, "Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa, hata hivyo ataishi. Amina. Mimi ndimi ufufuo na Uzima. Amina. Yeye aulaye mwili Wangu na kunywa Damu Yangu yuna Uzima wa Milele, nami nitamfufua, siku za mwisho." Kwa nini? Mwili, majivu, majivu ya volkano tuliyofanyiziwa, hutii amri Yake kwa kuwa Yeye ndiye Muumba wake.

153 Uhai ulioko ndani yetu sio tu Uhai umbaji, bali ni sehemu ya Uhai Wake mwenyewe. Hiyo ndiyo sababu tunayo mamlaka kunena na ibilisi, maana ni Uhai umbaji wa Mungu mwenyewe, ikiwa wewe umetiwa mafuta. Kwa njia sahihi. Si wewe, si wewe unayenena, bali Baba aishiye ndani yako. Unaona? "Usiwazie yale utakayosema, maana yataongezewa kwenye wakati huo." Endelea tu, dumu nalo. Loo, ninapenda jambo hilo!

154 Baada ya wale wanafunzi kujikuta mwishoni mwa safari yao, hapana shaka iliwafunukia baadhi yao, ya kwamba Yeye angali alikuwa pamoja nao. Baada ya wao kufika mwisho wa safari yao, hapana budi ilimfunukia mtu fulani, "Vema, hapa, hata hivyo, tulikuwa hapa tukitoa ushuhuda huu. Yule pale amelala, pale pale. Mnaona? Yeye anapumzika tu katikati ya miamsho. Nasi hapa tunazozana na kugombana, na kufadhaika kabisa, na kuvurugikiwa, na kutilia shaka, na kuhofu, kila kitu kingine. Naye Muumba amelala papa hapa chomboni." Loo, jamani!

155 Ee Mungu, jalia ifunukie baadhi yetu tena. Jalia itimie, Bwana, ya kwamba tunaweza kufahamu, tunaweza kuanza kufahamu.

156 Huyo ndiye Mungu yeye yule aliyekuchukua, akakutenganisha kutoka kwa mama yako. Mungu yeye yule aliyekupa Roho Mtakatifu! Yeye ni Mungu tu sasa hivi kadiri alivyokuwa wakati—wakati Yeye—wakati Yeye alipokupatia Roho Mtakatifu. Yeye yuko tu karibu nawe kadiri alivyokuwa

wakati huo. Vivyo hivyo hasa. Lazima ukumbuke, Yeye sikuzote yupo, daima. Hiyo ni kweli.

157 Iliwafunukia baadhi yao kwamba Muumba alikuwa pamoja nao chomboni.

158 Sijui usiku wa leo kama wagonjwa, kwa kuwa ninaenda kuzungumza na wagonjwa katika muda mfupi, kama inaweza kuwafunukia ya kwamba Mungu yeye yule mnayemtumaini, Muumba wa mbingu na nchi, Ambaye aliuumba mwili wako, yupo papa hapa. Yeye ni mkuu tu usiku wa leo kadiri alivyowahi kuwa. Yeye ni Mungu. Hawezi kuwa pungufu kamwe na abaki Mungu, mradi tu Yeye ni Mungu.

159 Mnasema, "Hiyo ni kweli, Ndugu Branham? Hayo ni Maandiko?"

160 Waebrania 13:8, "Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele." Naam. Yeye ni yule yule.

161 Kwa hiyo dua yetu inapaswa kuwa ni nini usiku wa leo, Ndugu Groomer, Ndugu Noel? Dua yetu ni nini? Kumwamsha Yesu. Iwapo kuna tatizo huku, hebu—hebu tumlete jukwaani. Amina. Tumwamshe Yesu, kwa kuwa tunaye pamoja nasi. Yeye yuko pamoja nasi, hakika, Yeye yuko, jinsi tu Yeye alivyowahi kuwa. Walikuwa tu ndio kwanza walione Neno la Kimaandiko ambalo Mungu alinena kumhusu, likithibitishwa na Yeye. Nasi pia tumeliona.

162 Mwajua, kwenye Siku ya Pentekoste, Petro, akivuviwa na Roho Mtakatifu, alisimama pale. Nao watu wote walikuwa wakicheka, wakilidhihaki kundi hilo dogo la Wayahudi huko nje, wakigugumiza maneno, na kutema mate, na kutoa udenda na kutenda kama kundi la walevi. Huku watu hao wakuu wa kidini wamesimama pale, wakisema, "Mbona, watu hawa wamejaa mvinyo mpya."

163 Ndipo Petro akasimama, nao wakachomwa moyoni mwao waliposikia mahubiri hayo aliyohubiri mhubiri huyo. Hakika aliielezea Injili kwa udhahiri. Akasema, "Ninyi watu wa Yuda, nanyi mkaao Yerusalemu, neno hili na lijulikane kwenu, na myasikilize maneno yangu. Hawa hawajalewa, kama mnavyodhani, kwa kuwa hii ni saa tatu mchana. Lakini hili . . . " "Labda"? La. "Hili ndilo lile lililonenwa na nabii Yoeli. 'Itakuwa katika siku za mwisho, asema Mungu, nitamwaga Roho Yangu juu ya wote wenye mwili: juu ya wana Wangu na watumishi Wangu wa kike na watumishi wanawake nitaimwaga Roho Yangu. Nitaonyesha maajabu katika mbingu juu, na moto na moshi. Na—na juu ya watumishi Wangu wanawake, nao watatabiri; na wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono.'" Kweli?

Nao wakasema, "Tufanyeje? Tutawezaje kuipata Hii?"

164 Yeye akasema, “Tubuni, kila mmoja wenu, mkabatizwe katika Jina la Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.” Nasi tunaambiwa na wengine kwamba hilo lililimaliza. Lakini wao, hiyo ni . . . Kama ukikomea hapo, hilo lingelimaliza. Lakini endelea mbele, yale Yeye aliyosema. “Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, watoto wenu, wale walio mbali, hata wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie.”

165 Mbele za ulimwengu baridi wa kimadhehebu, tunathibitisha kwamba hiyo ni Kweli. Amina. Ikiwa sehemu hiyo ya Neno ni kweli, mengine yote ya Hilo ni kweli. Naam. Wangeyaona Maandiko yakithibitishwa na Yeye. Tumeyaona, pia.

166 Hakuwa mgumu kuitwa kwenye jukwaa la utendaji. Ni rahisi sana kumwita Yeye. Mwangalie Yeye anapokuja kwenye utendaji, hata hivyo. Hilo ndilo ninalopenda, kumwona Yeye anapokuja katika umati wa watu. Mtazame wakati Yeye . . .

Wao walisema, “Bwana, tunaangamia.”

167 Akapangusa macho Yake, kasema, “Enyi wenye imani haba, kwa nini mlitilia shaka? Hivi hamjaona yote niliyofanya? Hivi . . . Hivi—hivi Maandiko hayajathibitishwa na Mimi? Maandiko yote yalielekeza Kwangu. Nanyi mmesema, wakati wote, mliniamini Mimi. ‘Naam, Bwana, tunakuamini. Tutafanya *hili*, *lile*, ama *linginelo*.’ Ndipo wakati tatizo dogo linapoinuka, ndipo mnaondoka.”

168 Hiyo si ni sisi leo hii? Hakika ndivyo. Kweli. Naam. “Mlisema mliniamini Mimi, bali kwa nini hamkuniamini? Kwa nini mkashuku?”

169 Mwanamke mmoja aliniambia, wakati fulani uliopita. Huenda niliru- . . . nilisema hilo hapa wakati mmoja. Litastahili kurudiwa. Alikuwa wa Sayansi ya Ukristo. Naye akasema, “Ndugu Branham, na—nathamini matamshi yako unayosema juu ya Maandiko. Ila,” kasema, “una kosa moja tu.”

170 Nikasema, “Asante. Ati moja tu? Jamani!” Nikasema, “Hakika nimepata neema machoni pako.”

171 Naye akasema, “Kosa hili ni, kwamba, unajivunia Yesu kupita kiasi.”

172 Nikasema, “Loo, jamani!” Nikasema, “Kama hilo ndilo kosa pekee nililo nalo, natumaini Mungu anajisikia—anajisikia nina kosa moja tu nifikapo huko. Basi kama hilo ndilo la pekee, nina hakika ninaingia.” Nikasema, “Kama ningalikuwa na ndimi elfu kumi, nisingeweza kumjivunia vya kutosha. Haijalishi ningesema nini, nisingeweza kumjivunia Yeye vya kutosha.”

173 Akasema, “Lakini, Ndugu Branham, unamfanya Yeye Mungu. Unamfanya Mungu.”

174 Nikasema, "Yeye alikuwa hivyo, na ndivyo alivyo. Na iwapo hakuwa hivyo, Yeye alikuwa mdanganyifu mkubwa sana ulimwengu uliyewahi kuwa naye." Hiyo ni kweli.

Akasema, "Loo! Usininii . . . "

Nikasema, "Hivi huamini hilo?"

175 Akasema, "Loo, Bw. Branham, ninaamini Yeye alikuwa ni mwalimu." Kisha kasema, "Ninaamini Yeye alikuwa ni nabii, lakini alikuwa tu ni nabii wa kawaida kama hao wengine."

Nikasema, "Loo, jamani! Loo! Umekosea sana."

Akasema, "Nitakuthibitishia hilo."

Nikasema, "Vipi?"

176 Akasema, "Katika Maandiko, wakati Lazaro . . . Yohana Mtakatifu, mlango wa 11, wakati Lazaro alipokufa, Biblia ilisema, ya kwamba, 'Yesu akalia.'" Basi akasema, "Angewezaje kuwa Mungu na alie?"

177 Nikasema, "Hiyo ilikuwa ni sehemu ya Mwanadamu ikilia. Huyo alikuwa ni Mwanadamu. Sehemu isiyopatikana na mauti ilikuwa ndani. Huyo alikuwa Mungu ndani Yake."

Akasema, "Aa, upuuzi!"

178 Nikasema, "Ninataka kukuuliza jambo fulani. Wakati, usiku ule kwenye ile meli, Yeye alikuwa ni Mwanadamu aliyejilaza pale, akilala usingizi. Hiyo ni kweli. Yeye alikuwa amelala na ni mchovu, kama mwanadamu. Lakini wakati alipoweza kuweka mguu Wake juu ya demani ya chombo hicho na kusema, 'Amani, tulia,' nazo pepo na mawimbi yakamtii. Huenda alikuwa ni Mwanadamu, akilia, bali wakati Yeye aliposema, 'Lazaro, njoo huku,' na mtu aliyekuwa amekufa siku nne akaja. Yeye alikuwa ni Mwanadamu wakati aliposhuka mlimani, akiona njaa ya chakula, akauangalia mti; bali alipochukua biskuti tano, na wawili, akawalisha elfu tano, huyo alikuwa ni Muumba." Hiyo ni kweli. Hakika.

179 Katika matendo, Mungu katika matendo! Loo, ninapenda hilo! Sio sanamu fulani, sio wazo fulani la uwongo la kuisugua sanamu, sio ufito fulani wa mzimu, bali ni Mungu halisi, aliye hai katika matendo. Amina. Amina. Sio kitu kilichokuwako. Kitu kilichopo sasa hivi. Linasikika la kijinga, kwa ulimwengu. Lakini, loo, jinsi lilivyo zuri, kwa mtakatifu anayeamini. Ni ajabu jinsi gani! Bila shaka. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

180 Mwajua, Yeye alikuwa ni zaidi ya nabii, na hata hivyo Yeye alikuwa ni Nabii. Alikuwa ni Mungu-Nabii. Mnaona? Kwa sababu, manabii walikuwa ni Neno. Biblia ilisema ya kwamba Neno lilimjia nabii, na mradi tu nabii alikuwa akinena Neno, kwamba yeye na Mungu walikuwa . . . Mtu huyo hakujua alilokuwa akifanya. Alikuwa tu akinena Neno la Mungu. Mnaona? Pasipo kujua alilokuwa akifanya, alikuwa akitabiri

chini ya uvuvio. Mnaona? Basi, halikuwa ni neno la mtu huyo. Lilikuwa ni Mungu akinena kupitia kwa midomo.

181 Sasa, Mungu alichagua kumtumia mwanadamu. Sasa, Yeye angeweza kuchagua kutumia jua kuihubiri Injili. Angeweza kuchagua kutumia upepo kuibuhiri Injili. Angeweza kuchagua nyota. Angeweza kuchagua chochote alichotaka kuchagua, bali Yeye alimchagua mwanadamu.

182 Na mtu fulani atafanya hivyo. Hiyo ni kweli, mtu fulani. Kama angaliweza tu kujipatia mtu, mtu mmoja ambaye Yeye angeweza kumshika mkononi Mwake, Yeye atafanya hivyo. Amekuwa na wakati mgumu sana, kumpata mtu mmoja.

183 Ninawazia juu ya Samsoni. Yeye alimpata mtu mwenye nguvu nyingi sana. Naye Samsoni alimtolea Mungu nguvu zake, bali asingemtolea moyo wake. Alimpa huo Delila. Mnaona?

184 Mungu anataka moyo wako, nguvu, nafsi, mwili, akili, yote uliyo nayo. Ndiyo njia pekee Yeye anayoweza kukutumia, kuutumia utu wote. Naam.

185 Hivyo ndivyo Yesu alivyokuwa. "Ndani Yake mlikaa utimilifu wote wa Mungu kwa jinsi ya mwili." Tunao kwa kipimo.

186 Kwa sababu, wakati Nguzo hiyo ya Moto iliposhuka Pentekoste, mnaona, Biblia ilisema, "Ndimi zilizogawanyika kama Moto ziliwakalia juu yao." Ilikuwa ni kitu gani? Nguzo hiyo ya Moto ikijigawa Yenyewe, na kujigawa Mwenyewe miongoni mwa watu Wake. Ni jambo lenye fadhili jinsi gani! Mnaona? Mungu ndani yako? Mnaona? Mungu ndani ya watu Wake. Sasa angalieni.

187 Mtu fulani anasema sasa, kanisani usiku wa leo, angesema hivi. Watu leo hii, kama ungesema, "Laiti tungaliweza tu kujua Yeye yupo hapa pamoja nasi. Kuna njia yoyote?"

188 Mnaona, wangeweza kumwangalia Yeye. Sasa, sikilizeni kwa makini sasa, kabla hatujaitisha mstari wa maombi. Wangeweza kumwangalia na kusema, "Yule *pale* amelala, chomboni. Sasa, Yuko *pale*."

189 Sasa, laiti tungalikuwa tu na njia ya kufanya kitu kama hicho. Kama tungeweza tu kumwangalia Yeye mahali fulani, tungeweza kusema, "Yule pale, pale *pale*."

190 Sasa, lakini Yeye yuko karibu hivyo. Hata yuko karibu zaidi. "Kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari." Hiyo si ni kweli? Yeye yuko karibu zaidi kuliko alivyokuwa kwao, sababu ilibidi waende kwenye—kwenye sitaha ya chombo, na kurudi huko nyuma, na kumwamsha. Haikubidi kufanya hivyo. Loo, jamani! Whiu! Loo! Ninajisikia kubarikiwa sasa hivi. Ninaanza tu kujisikia vizuri sana, sasa hivi. Loo!

191 Waebrania 13:8 inasema, “Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele.” Naye alisema tena, “Tazama, niko pamoja nanyi sikuzote, hata mwisho, wakati wa jioni.” Nilihubiri hayo jana usiku. “Wakati wa jioni, ningali nitakuwako.” Tena, “Kamwe sitawaacha. Haijalishi chombo kinafanya nini, jinsi wanavyoyumbayumba na kubingirika, ama chochote kingine, nitakuwa pamoja nanyi, nitakuwa pamoja nanyi hata wakati wa mwisho, kamwe sitawaacha.”

Unasema, “Hili linawezekanaje, Ndugu Branham?”

192 Yohana Mtakatifu, wa 12. . .mlango wa 14, kifungu cha 12, ilisema ya kwamba Yeye angelithibitisha. Mnaona? “Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye naye atazifanya.”

193 Unasema, “Laiti ungeweza kunithibitishia na kunionyesha ya kwamba Yeye yuko tu kama vile alivyokuwa sikuzote. Laiti ungaliweza kunithibitishia!”

194 Vema, *hapa* ndipo Yeye alipotoa changamoto, lile thibitisho. “Yeye aniaminiye Mimi, mambo niyafanyayo Mimi.” Kwa maneno mengine, utakuwa Masihi mdogo, Kijimasihi. Hiyo ni kweli kabisa. Kwa kuwa Uzima Wake ukiwa ndani yako, sio wewe; ni Yeye. Unaona? Nawe umechaguliwa kuendeleza kazi Yake. “Yeye aniaminiye Mimi, nitathibitisha kwamba Mimi ni Masihi. Na yeye aniaminiye Mimi atafanya jambo lile lile.” Sasa, hiyo, Yeye hawezi kusema uongo na awe yale unayomwazia kuwa, na vile ninavyojua Yeye alivyo, na unavyoamini alivyo, pia. Unaona?

195 Unajua anafanya nini? Yupo hapa usiku wa leo, akingojea kuthibitishwa. Hiyo ni kweli. Mnajua kile tunachopaswa kufanya? Tunapaswa kufanya kama wao. Kumwamsha Yesu aliye ndani yetu. Kumwamsha Yesu katika maisha yetu wenyewe: Mungu aliyeziwasha moto nafsi zetu kwa Roho Mtakatifu; Mungu aliyeyachukua macho haya yangu yaliyopofushwa, akayafungua; Mungu yule aliyeniinua kutoka kwenye kitanda cha mauti. Mungu niliyemwona akiwafufua wafu, baada ya kufa kwa saa kadhaa; daktari alitangaza “amekufa,” na kuandika taarifa yake, mara tano mbalimbali. Mwamsheni Mungu huyo. Mwamsheni. Inatupasa kumwita Yesu na kumwamsha, na kumwita jukwaani. Tunamhitaji. Naam, bwana.

196 Kisha, tumwite, kulithibitisha Neno Lake. Kama tukimwamsha, tumwamshe, ndani yetu, mpaka mashaka yako na kuchanganyikiwa kumetoweka. Sasa mwite Yeye na kusema, “Bwana, Wewe uliahidi, muda kidogo na ulimwengu hautakuona tena. Na mimi si wa ulimwengu. Uliomba ya kwamba sitakuwa wa ulimwengu, wala mimi si wa ulimwengu. Mimi ni Wako. Na Wewe ulisema, ‘Ulimwengu hautaniona tena, hata hivyo ninyi mtaniona.’ A-ha. ‘Mtaniona.’ Bwana, ninataka kukusumbua. Ninataka kukuamsha, kutoka kwenye mwili

wangu mwenyewe uliolala, moyo wangu mwenyewe uliolala, wa kweli hizi." Mwamsheni Yesu. "Njoni kwangu." Ndipo mashaka na hofu zitakwisha.

197 Kuchanganyikiwa kwote na hofu, kuhusu, "Loo, daktari alisema *hivi*, na kwamba atafanya *hivi*. Wala si—si—sijui nitakalofanya. Ni—ni . . ." Yote yatakoma tu, maana Yeye ni Mungu. Yeye hunena, na kila kitu kingine kinatulia.

198 Sasa, tungeweza kuendelea kuzungumza, pamoja na kurasa zingine nyingi za muhtasari. Bali hebu niwaulizeni jambo fulani sasa, maana ni karibu sana, yapata saa tatu kasoro dakika kumi. Bila shaka, hizo ni saa mbili mapema kuliko jana usiku, mwajua, pia. Lakini, angalieni, hebu niseme hivi, kusimama sasa hivi, nami naweza kumalizia hili wakati mwingine.

199 Mungu anaweza kushindwa? [Kusanyiko linasema, "La."—Mh.] Wala na Neno Lake, kwa sababu Yeye ni Neno Lake. "Hapo mwanzo alikuwako Neno, huyo Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Naye Neno akafanyika mwili akakaa miongoni mwetu." "Bado kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, bali ninyi mtaniona Mimi. Kwa kuwa Mimi . . ." Na *Mimi* ni kiwakilishi nafsi. "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hata ukamilifu wa dahari, mwisho wa wakati. Kwenye wakati wa mwisho, nitakuwako." Hiyo nuru itakuwa ikiangaza kwenye wakati wa mwisho.

200 "Ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Waebrania 13:8 imeandikwa. Mnaamini hilo? Waebrania 13:8, imeandikwa. Kwa hiyo, kama imeandikwa, sasa na itimie. Amina. Usiogope kuliweka Neno Lake kwenye jaribio. Lipo hapo. Yeye yupo hapa. Jambo pekee unalopaswa kufanya ni kumwamsha. Wewe . . .

201 Tunavuta kwa wingi sana roho isiyochujwa, nyingi sana kutufanya kujaribu kukumbuka jambo lingine, na kugeukia, "Mimi nimechoka. Ni—ni mchovu kupita kiasi. Nimeona *hili* likifanywa." Kwa nini kurejea kwenye kitu kilichoharibika? "Nitakupeleka kwenye . . ." Kasema, "Ninamjua mtu fulani, alimtumainia Mungu, na akafa."

202 Ninajua mamilioni, wakati uo huo, waliokufa chini ya uangalizi wa madaktari. Mnaona? Hakika. Hakika. Ikiwa daktari amefanya yote awezayo kufanya, huna lingine ila kumtumainia Mungu, na kama utaliamini.

203 Sasa, huwezi tu kusema, "Vema, ni—nitamtumainia Yeye." Hilo silo. Hilo ni, lifanye kweli. Hilo silo.

204 Inakupasa kumsumbua, mpaka unapoweza kumwona Yeye akiingia. Hivi maombi yetu hayawezi kumsumbua? Hivi maombi yetu hayawezi kumwamsha kutoka kwenye raha Yake, yamlete jukwaani? Walimwamsha. Walilia, "Bwana, tunaangamia," ndipo Yeye akajitokeza jukwaani. Sasa tunaweza kufanya jambo lilo hilo. Sasa, mnaamini hilo?

Basi hebu tuombe.

205 Ee Bwana, wazo hili dogo rahisi, "Mwamshe Yesu." Bwana, hatuja—hatujamtumia Roho Wake na imani Yake, kwa muda mrefu sana, mpaka anaenda tu kulala, tuseme, nafsini mwetu. Jalia tujitikise usiku wa leo. Jalia tujiamshe na kujiondolea usingizi wetu wenyewe kutoka kwetu, tupate kuona ya kwamba Yeye angali katika chombo.

206 Ee Bwana, leo hii nilijaribu kuitikisa nafsi yangu. Nilijua ilinibidi kusimama mbele ya kundi dogo la watu hapa juu usiku wa leo. Nami ninajitikisa. Bwana Yesu, amka, njoo huku. Nimeliweka Neno Lako mbele za hawa watu. Limeletwa kwenye jaribio. Lithibitishie kusanyiko hili usiku wa leo, Bwana, ya kwamba Wewe ungali hai, ya kwamba ungali hapa pamoja nasi. Maneno Yako ni kweli, "Niko pamoja nanyi sikuzote, hata mwisho wa ulimwengu." Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele. Ungali kwenye meli, Bwana, ile meli ya kale ya Sayuni inayotubeba kuvuka bahari zilizochafuka. Ndipo wakati ibilisi anapovumisha dhoruba juu yetu, inaleta tofauti gani, mradi tu Yeye yuko ndani ya meli? Kuwa pamoja nasi sasa, Baba. Pia naomba uingie moja kwa moja ndani ya mioyo ya watu usiku wa leo.

207 Naomba uingie katika moyo wangu, nafsi, mwili, nia, macho, midomo. Na ujalie kujitolea huku, kwa nafsi yangu, kuwe ni thibitisho la Neno Lako, ulililoahidi katika Yohana Mtakatifu 14:12. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi wewe nawe utazifanya."

208 Basi jalia iwe kwamba, uende kwenye kusanyiko, wapate kuliamini jinsi *hii,* "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi." Ndipo wakati tukiketi kwenye mahali hapa pa Mbinguni usiku wa leo, katika Kristo Yesu, ujidhihirishe Mwenyewe, Bwana. Ni ahadi Yako. Maneno Yako hayatashindwa. Halafu basi, hakika, basi acha liwe juu ya misingi ya imani ya hawa watu, ili waweze kukupokea Wewe basi. Hayo ndiyo yote tuwezayo kufanya.

209 Ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utajipatia Mwenyewe utukufu. Ninalikabidhi kusanyiko hili, Ujumbe, Mbegu ambayo imepandwa. Jalia Roho Mtakatifu aingie, aangaze nuru Yake. Kama nilivyosema juu ya mbegu ya maskini mwanamke yule Msamaria; jalia, upesi, mara tu hiyo Nuru inapoangaza, jalia mwaminio aione. Jalia mwanamume mgonjwa aione, mwanamke mgonjwa, mvulana, ama msichana. Na hao walio na shauku kwa ajili ya wengine, jalia waione, upesi, na waponywe. Katika Jina la Yesu. Amina.

Mnaamini sasa?

210 Sasa, ninaamini. . .Kadi za maombi? Vema, nitajaribu. Siwezi kuleta ila wachache tu kwa wakati mmoja, kwa hiyo hebu

tuanze kuwaleta huku, baadhi ya watu, kuwaombea. Na sasa ninajua tumesongamana sana.

211 Kaeni tu kimya, ndugu wahudumu. Nitarudi nyuma papa hapa juu, dhidi yake. Chukueni mahali pe—penu hapa. Vema.

212 Sasa, usitilie shaka. Amini. Utafanya hivyo? "Mambo yote yanawezekana kwao waaminio." Hiyo ni kweli. "Mambo yote yanawezekana kwao waaminio." Vema. Sasa, huna budi kuamini. Huna budi kuliamini Neno la Mungu kwamba ni Kweli. Vema. Sasa hebu . . .

213 Ni wangapi tunaoweza kuwasimamisha hapa kwa wakati mmoja, kama wanane, kumi? Vema.

214 Hebu tuanzie kutoka namba moja, na tuchukue namba moja hadi yapata kumi ama kumi na tano, A. A, namba moja hadi kumi na tano. Ni nani aliye na kadi ya maombi A, namba moja?

215 Ninaona kuna Wahispaniola na Wahindi pia hapa usiku wa leo. Huenda wasiweze kulielewa.

216 Vema, huyu hapa mwanamke mmoja anakuja, papa hapa. Namba mbili? Papa hapa. A-ha. Papa *hapa*. Naam. Papa hapa. Vema. Namba mbili. Tatu, namba tatu? Vema, papa *hapa*, tafadhali. Namba nne, tano, sita, saba, nane? Naomba mtu fulani amchukue huyo mvulana mdogo hapo, asije akakanyagwa. Nane, tisa, kumi. Sasa, yapata kumi. Vema. Tutaona jinsi kwa namna fulani . . . Loo, sisi ni . . . Sijui. Huenda—huenda nikawa na wengi kupita kiasi sasa. Vema. Kumi. Hilo ni sawa. Acheni wapange mstari moja kwa moja namna hiyo. Hilo ni sawa.

217 Ni wangapi wanaamini sasa kwa moyo wako wote? Sasa, hatuna wengi mno hapa, kumi. Kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Vema.

218 Sasa, kila mmoja, ninawatakeni mwe na kicho kabisa. Sasa, nimetumia saa moja kamili, ama zaidi kidogo, nikizungumza. Ninayosema hayamaanishi kitu isipokuwa Mungu ayaunge mkono. Na asipoyaunga mkono, mnaona, Neno lingali ni kweli, naam, haijalishi kama anayaunga mkono ama la. Amefanya hivyo hapo awali, mnaona, na Yeye kamwe hajawahi kunipungukia. Na mimi—mimi najua Yeye hatanipungukia, kwa sababu Yeye alisema hatanipungukia. Mnaona? Nami na—najua atafanya hivyo. Lakini hatuna budi kuamini. Kwa mioyo yetu yote, hatuna budi kuamini. Sasa, nijuavyo mimi . . .

219 Nawatakeni ninyi mlio kwenye mstari wa maombi, mwangalie upande huu, wale wote watakaokuwa kwenye mstari wa maombi. Ni—ninaamini ya kwamba kila mmoja wao ni wageni kwangu. Ninaamini wote ni wageni. Kama hiyo ni kweli, inua tu mkono wako. Ikiwa siwajui ninyi nyote, inueni tu mikono yenu namna *hiyo*. Vema. Mnaona? Sasa, siwajui watu hao. Wao, hawapo wengi hapa . . .

220 Ninawajua wengine hapa katika mistari hii papa *hapa*. Sina hakika. Nafikiri huyu ni mke wa Ndugu Noel. Sina hakika. Imekuwa ni muda mrefu.

221 Na kwa hiyo Ndugu Johnson yukoje? Nafikiri ana kiharusi, sivyo? Loo, jamani! Wasemaje? Hiyo ni kweli? Nautakia heri moyo wake. Watu hao walikuwa kama baba na mama kwangu, nilipoanza mkutano kwa mara ya kwanza, kundi hili dogo la watu wa Arkansas. Kamwe sitasahau Arkansas. La, bwana. Sijawahi kuwa kwenye mkutano mahali popote, pasipokuwapo na wengi sana wa "Arkie." Ni wangapi waliopo hapa usiku wa leo, inueni mikono yenu, kutoka Arkansas? Sasa, hao wengine wametoka Oklahoma, kwa hiyo unaweza tu kutegemea hilo. Mnaona? Hivyo ndivyo inavyoenda. Lakini sisi sote tunaelekea Mbinguni, mnaona, "tumeketi pamoja katika mahali pa mbinguni katika Kristo Yesu."

222 Dada Jones na Ndugu Jones, miaka kadhaa iliyopita wakati nilipokuja kanisani mwenu, ninaamini ilikuwa ni Moark. Sivyo? Nanyi mnakumbuka wakati nilipokuja huko, njia pekee niliyojua ya kupata shida za watu ilikuwa ni kwa. . . Mngewaongoza jukwaani nao wangeweka mkono wao juu ya wangu, kisha ningengojea pale kwa dakika moja tu. Halafu basi, bila kujaribu kutumia sauti yangu mwenyewe, na Yeye angenena, aseme, "Kivimbe, mtoto wa jicho." Na niliwaambia kwamba ungekuja wakati ambapo, Yeye aliniambia kule juu, kama ningekuwa mwaminifu, basi ningejua siri yenyewe ya moyo wao. Mnaona? Hiyo ni kweli. Ni wangapi wanaokumbuka hilo wakati nilipokuja Phoenix kwa mara ya kwanza? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema. Imetukia? ["Amina."] Mnaona?

223 Sasa, kumbukeni. Angalieni kanda hii. Tunapiga hatua moja kwa moja juu zaidi kidogo sasa. Mnaona? Inapanda moja kwa moja juu, juu zaidi kidogo. Kumbukeni hilo. Ku—kumbukeni tu. Mnaona?

224 Sasa, tunataka kumwona Yesu. Ninataka kumwona Yeye. Sasa, tunajua ya kwamba mwili Wake hautarudi duniani mpaka atakapokuja kwa ajili ya Kanisa, kwa sababu hauna budi kubaki Kule kwa ajili ya dhabihu. Hiyo ni kweli? Hauna budi kuwa madhabahuni. Yeye ameketi kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, usiku wa leo. Nao hauna budi kubaki kule, kwa kuwa, kwa kupigwa Kwake, Yeye ni Dhabihu, nayo Dhabihu iko juu ya madhabahu. Mnaona? Wala mwili Wake hauwezi kuja. Lakini uhai Wake ulirudi, uliokuwa ndani ya Kristo, ulirudi juu ya kanisa, katika umbo la Roho Mtakatifu. Naye Roho Mtakatifu. . .

225 Mwili huo sio uliofanya hilo, hata hivyo. Yeye alisema, "Si Mimi nizitendaye hizo kazi. Ni Baba Yangu anayekaa ndani

Yangu, Yeye anazitenda hizo kazi." Sasa, tunaamini jambo hilo. Sivyo?

226 Sasa, kama niliwaambia ya kwamba Roho ya jambazi iko ndani yangu, mngenitarajia kuwa na bunduki kubwakubwa, na ni katili. Mnaona? Roho ya mwanasanaa, mngenitarajia kuchukua burashi na kutia rangi.

227 Kama nikiwaambia, "Roho wa Kristo," basi atafanya kazi za Kristo. "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi . . . " Ni kama tu kutia uhai kutoka kwa mzabibu mmoja hadi mwingine, utazaa tu—tunda la uhai ulioko ndani ya huo mzabibu.

228 Sasa, sijui kwamba Yeye atafanya hili. Siwezi kusema. Lakini ikiwa mimi, kwa karama . . . Sasa, hakuna haja ya kujaribu kulielezea. Siwezi.

229 Lakini wengi wenu mnajua ya kwamba nimekuwa kote uliwenguni, nimekuwa huko, mara kadhaa. Mbele ya watu nusu milioni, wakati mmoja, watu laki tano. Nimeona lugha nyingi sana mbalimbali, ilinibidi kuandika yale niliyosema, nipate kungojea mpaka lipitie kwenye wakalimani kumi na watano zaidi, kisha nirejee kwenye jambo nililosema. Na kumwona huyo Roho wa Mungu akishuka moja kwa moja kule chini na kufanya jambo lile lile analofanya hapa. Mnaona? Mnaona? Mataifa yote, lugha, pasipo na udhuru.

230 Sasa, kumbukeni, halitaenda kwa kila mtu. Wakati Yesu alipokuwa duniani, si zaidi ya theluthi moja ya jamii ya Kiyahudi ilijua Yeye alikuwa duniani. Mnajua jambo hilo. Yeye alikuja kwa Wateule, nao wakampokea. Hiyo ni kweli. Huko ndiko Roho anakoenda usiku wa leo, kwa Wateule.

231 Sasa, kama unaweza kuamini ya kwamba Yesu alikufa kwa ajili ya dhambi zako, nawe umemkubali Yeye kama Mwokozi wako, na Yeye ameyachukua maisha yako na kuyafinyanga tena, basi, kumbuka, "Kwa mapigo Yake sisi tuliponywa." Mnaona? Sasa, mliponywa. Mmeponywa tayari. Mnaamini jambo hilo? Sasa, Biblia ilisema, "Tuliponywa." Hiyo ni kweli? Sio "tutaponywa." Sisi, tayari. Tumeponywa, tayari.

232 Suala lote la dhambi lilitatuliwa wakati Yesu alipokufa pale Kalvari. Unaamini hilo, ndugu? Mnaona? "Yeye ni Mwana-kondoo wa Mungu aziondoaye dhambi za ulimwengu." Sasa, kamwe halitakufaa kitu mpaka uukubali msamaha wako. Unaona, huna budi kuukubali. Pia inakubidi kuukubali uponyaji wako vivyo hivyo.

233 Kama mtu fulani akipitia hapa, aseme, "Nitakuponya," sasa, yeye amekosea. Hiyo ni kinyume na Maandiko. Yeye anaweza kukuonyesha hapa ambapo Yesu alifanya hilo kwa ajili yako, nalo limewekwa msingi juu ya imani yako. Mungu kamwe hawezi kufanya lolote . . . Mungu hawezi kutenda kazi kinyume na imani yako. Huna budi kuamini.

234 Sasa, Yesu, wakati alipokuja kwa watu Wake mwenyewe, sikilizeni yale Biblia iliyosema. “Kazi nyingi kuu asingeweza kufanya, kwa sababu ya kutokuamini kwao,” baada ya kujionyesha kuwa Masihi. Sasa, Yeye alithibitisha hilo katika siku hiyo, alikuwa ni Masihi.

235 Mungu na anisaidie kuinyenyekeza roho yangu hivi kwamba ninaweza kuthibitisha kwamba Yeye angali ni Masihi; kwamba, Mungu yeye yule aliyekuwa duniani, anaweza kuuchukua mwi—mwili unaopatikana na mauti, ajisalimishe Kwake, na kutenda kazi kupitia huo vile vile hasa Yeye alivyoahidi kufanya. Hilo si lingeshawishi? Hivi hilo si lingekuwa likionyesha kwamba Yeye—Yeye hajalala usingizi? Yu macho. Yeye yuko tayari kwako kumwita kazini.

236 Sasa vipi kuhusu mimi kusimama hapa, usiku wa leo, nina kazi gani? Kunao watu mia moja na hamsini hapa, nakisia, kitu kama hicho. Kama ni mia moja na hamsini, kama ni mtu mmo—mmoja, walikuwa laki tano, haileti tofauti yoyote. Ni mamoja tu. Mnaona?

237 Sasa, kama mtu yeyote anawazia kwamba hili ni la bandia, na si kweli, nakuomba upande uje upachukue mahali pangu na kufanya jambo lile lile. A-ha. Naam. Mnaona? Unajua vema kuliko kujaribu hilo. A-ha. Mnaona? Angalieni. Lakini, sasa, Mungu hana budi kuthibitisha kama Yeye ni sahihi ama la. Sasa, kama Bwana Mungu . . .

238 Huyu ni mmoja wa . . . Mpe mvulana yule kadi yako pale. Njoo hapa. Huyu hapa mama mmoja, mdogo sana kuliko mimi. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Nadhani hatufahamiani? Hiyo ni kweli. Hatufahamiani sisi kwa sisi.

239 Sasa, mtakapoenda nyumbani, someni Yahana Mtakatifu, mlango wa 4, na mwone kama hapa hata si mahali padogo mduara . . . Yupo mtu yeyote aliyepata kuwa Palestina, huko—huko juu Sikari? Maskini kisima kile kingali pale ambapo mwanamke yule alipokuwa; mahali padogo mduara, penye mizabibu. Basi Yesu aliketi kuegemea ukuta wakati yule mwanamke alipotokea. Alikuwa amesimama katika mandhari ndogo wakati yule mwanamke alipojitokeza kutoka mtaani hapa chini, akaja na kuchota maji, mwishoni mwa mtaa. Naye alikuja pale juu. Basi sasa aliendeleza mazungumzo naye mpaka akapata mahali shida yake ilipokuwa, ndipo akamwambia shida yake ilikuwa nini.

240 Basi alipofanya hivyo, yeye alisema, upesi, “Bwana, hapana shaka Wewe ni nabii, unaona, maana Wewe . . . ” Ilibidi awe na . . . Basi kama Yeye alikuwa ni nabii, hilo lilikuwa ni Neno la Mungu likimjia. Lakini yeye alisema, “Tunajua tunamtazamia Masihi. Naye atakapokuja, hivyo ndivyo Yeye atakavyofanya.” Ni wangapi wanajua hayo ni Maandiko? Hayo ni Maandiko.

241 Sasa, huu hapa mkono wangu juu ya Biblia. Mimi, kadiri nijuavyo mimi, sijawahi kumwona huyu mwanamke maishani mwangu. Naye anasema hatufahamiani kabisa. Sasa, Neno ama linapaswa kuwa kweli ama si kweli. Kweli. Ama ni kweli au uongo. Hatuwezi kulifanya kitu kingine tofauti.

242 Sasa, mama, kuzungumza tu na wewe kwa dakika moja, kama Bwana wetu alivyofanya na yule mwanamke. . . Kama anaweza kuniambia . . .

243 Sasa, kama ningekwambia, "Loo, hakika, ulikuwa na kadi ya maombi. Umekuja hapa juu. Wewe ni mgonjwa." Unaona? Vema, basi kama ningesema, "Utukufu kwa Mungu," niweke mikono yangu juu yako. "Utukufu kwa Mungu, utapata afya." Ni sawa, hakuna chochote kibaya na hilo. Hilo ndilo jambo la kufanya hasa. Mnaona? Hiyo ni kweli.

244 Biblia ilisema, "Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Hiyo ni kweli.

245 Lakini sasa, ungeweza kukuna kichwa chako na kutafakari, "Hivi yeye aliniambia kweli? Nitapata afya?"

246 Sasa, vipi kama—kama kile kitu Fulani kinachoyajua maisha yako, vile umekuwa, yale uliyofanya, na, ama shida yako, kama alivyomwambia yule mwanamke shida yake ilivyokuwa? Basi kama angeweza kukwambia mambo hayo, vema, hakika kama Yeye anajua yale yamekuwako, Yeye anajua yale yatakayokuwako. Hiyo ni kweli? Hakika.

247 Sasa, ikiwa huyu mwanamke ni mgonjwa. . . Huenda ikawa anasimama kwa ajili ya mtu mwingine. Huenda ikawa ni maradhi. Huenda ikawa ni matatizo ya kifedha. Huenda ikawa ni matatizo ya kinyumbani. Sijui. Siwezi kukwambia. Hiyo ni kweli. Unaona? Lakini hata iwe ni nini, kama Yeye angeweza kuitaja, yeye angejua kama ni kweli ama si kweli. Yeye angeijua. Unajua kama ilikuwa hivyo ama sivyo. Ndipo kama si kweli, basi huyo hakuwa ni Roho wa Mungu, maana nabii amesema hivyo, nao unabii wake ulikuwa si sahihi. Lakini kama ni kweli, basi huyo alikuwa ni Roho wa Mungu. Mnaona?

248 Sasa hilo si lingetufariji na kutufanya kujisikia vizuri sana, kama tunajua kwamba Yesu alikuwa hapa pamoja nasi usiku wa leo? Ingewapa imani? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Mnaona? Bila shaka.

249 Sasa, kumponya mwanamke huyu, nisingeweza kufanya hilo. Si—siwezi kufanya hilo. Imetendeka tayari. Mnaona? Mnaona? Imetendeka, na sasa inategemea imani yake kuliamini. Sasa, kama Yeye alikuwa amesimama hapa, Mwenyewe, akiwa amevaa suti hii, asingeweza kumponya. Yeye angesema amelifanya tayari. "Kama unaweza kuamini, unaona, kwamba nimelifanya, limekwisha." Unaona? Jambo ndilo hilo. Unaona?

250 Lakini, sasa, jambo pekee angaliweza kufanya, Yeye angeweza kuthibitisha kwamba alikuwa ni Masihi, hata hivyo, yule Mungu-Nabii ajaye. Naye aliahidi kwamba wanafunzi Wake wangefanya jambo lile lile, kwa hiyo haya basi. Mnaona? Inayarudisha moja kwa moja kwenye Maandiko. Na hayo ni Maandiko, ndugu zangu. Ninajua yote ni kinyume na imani ya kisasa, bali ni imani ya Mungu. Ni njia ya Mungu, maana Yeye alisema hivyo. Hayo hapo Maandiko ya kujisomea mwenyewe. Wanajaribu tu kuyapindua na kufanya kitu kingine kutoka kwake.

251 Sasa, nataka kuwaulizeni jambo fulani. Huyu Mwanamke ni mwaminio. Ninataka ku . . .

252 Jambo fulani litatukia. Ninyi kumbukeni tu, jambo fulani litatukia. Sasa, kama likitukia, basi ni wangapi watakaokubali na kusema, "Hilo lilitosha kwangu mimi"? Utaamini hilo, mama? Mnaliamini, upande *huo*? Wengine wenu mnaliamini? Mungu na awe hakimu.

253 Sasa, si zaidi ya nilivyosema hilo, sababu ya mimi kusema hivyo. Ni wangapi waliopata kuiona hiyo Nuru, ile picha ya Nuru hiyo, yule Malaika wa Bwana? George J. Lacy, mwajua. Mnaona? Vema. Nuru hiyo iko kati yangu na yeye, sasa. Nayo ni ya makaribisho. Ninajua yeye ni mwaminio. Hiyo ni kweli.

254 Kile unachotaka nikuombee kukihusu: vidonda, vidonda mwilini mwako. Jambo lingine, ni matatizo tu. Unayo mambo mengi sana. Lakini, ngoja kidogo. Ninawasiliana na roho yako. Uko tayari kwa upasuaji. Hiyo ni kweli. Umepangiwa upasuaji. Sasa, Yeye alisema huo ulikuwa katika kibofu nyongo. Hiyo ni kweli. Sasa unafikiri nini? Mungu akubariki. Amini tu. Jambo ndilo hilo. Amina.

255 Yeye si ni Kristo? Sasa mwulizeni mama huyo mkitaka. Hiyo ni . . . Mnaona?

256 Sasa, huyo ni Yeye jana, leo, na hata milele. Mnaona? Imani yenu imemwamsha sasa. Mnaona? Yeye yuko jukwaani, kufanya mambo ya kuwasaidia, kuwabariki, na kuwapa vitu hivyo mnavyotamani kuwa navyo.

257 Sasa, ono hilo moja limenidhoofisha sana kuliko mahubiri hayo ya saa moja na nusu. Mnaona? Na unajisikia tu ukitetemeka, ukiondoka. Mnaona? Kwa kweli, hii ndiyo mara ya kwanza nimekuwa na ibada . . .

258 Hivi majuzi usiku, Roho Mtakatifu alishuka, juu ya kanisa fulani, ninajua, na akawaita watu watatu au wanne. Basi alipowaita, wao hawakuitika upesi tu, ndipo basi akahuzunika. Papo hapo akaondoka, mnaona, na kuniacha papo hapo. Huna—huna budi kujibu, inakupasa kumjibu Huyo. Naam, bwana. Kumbuka tu, Yeye hawajibiki kwako; wewe unawajibika, Kwake.

259 Hatufahamiani. [Dada, anasema, "Nimekuona mara moja."—Mh.] Uliniona mara moja. ["Ndiyo."] Hapa Arizona? ["Ndiyo. Nilikuwa . . . ? . . . kwenye mstari wa maombi."] Katika mstari wa maombi. Hiyo imekuwa ni muda gani? ["Ilikuwa ama ni '54 ama '55."] Naam. Muda mrefu uliopita. Naam, bwana.

260 Ninakumbuka mstari wa maombi ulio mrefu zaidi niliowahi kufanyiza maishani mwangu, ulikuwa hapa chini Phoenix, alasiri moja. Juu . . .

261 Ninasahau jina la kanisa hilo. Kulikuwa na . . . Ilikuwa, maskini jamaa mfupi, alikuwa na kanisa. Ninasahau kile yeye . . . Kanisa kubwa mno, hapa Phoenix. Ilikuwa ni Fuller? La. Ndugu Fuller, ninamjua. Wasema nini? Ninamkumbuka Garcia. Lakini hili ni kanisa kubwa mno kule ambako Dk. Sutton alikuwa ndiye mchungaji, ama kitu fulani. Jina la kanisa hilo kubwa kule lilikuwa ni gani? Ni moja ya makanisa makubwa zaidi ya full Gospel nchini. [Mtu fulani anasema, "Faulkner."—Mh.] Faulkner, hilo ndilo. Hilo ndilo, Faulkner, kule kanisani mwake.

262 Mnaukumbuka mstari huo? Nilianza alasiri hiyo, nikaomba mpaka usiku wa manane usiku huo, ninaamini ndivyo ilivyokuwa. Kuninii tu . . . Kuwawekea tu watu mikono, nilidhoofika sana hata nisingeweza kusogea tena, ni vigumu. Mnaona?

263 Hiyo ilikuwa ni kabla ono halijakuja. Lingekuja, bali kwa nadra tu, mara kwa mara. Halafu mara nyingine wakati ningekuwa peke yangu, Yeye angeniambia jambo fulani lilikuwa linaenda kutukia. Ningekuja niwaambie ninyi nyote kwamba Yeye aliniambia kitu fulani kilikuwa kinaenda kutukia. Daima kilitukia. Sivyo? Naam. Sasa, Hilo linasema nini? "Liamini." Mungu hulithibitisha. Mnaona?

264 Sasa, huyu mama, kwa kuwa ni miaka mingi iliyopita, ninakisia nimewaombea watu milioni mbili na nusu, ama labda, tangu wakati huo, mwajua, kote ulimwenguni. Labda zaidi ya hao. Lakini kamwe ni—nisingejua ni nani, kukuhusu wewe, ama lolote kulihusu. Lakini sasa Biblia ilisema, ya kwamba, wakati mmoja . . .

265 Na, jambo lingine, giza hilo, lililokuwa juu ya mwanamke huyo, limemwondokea. Hiyo ni kweli. A-ha. Ninajua. Unajisikia tofauti, sivyo? Kama ukiishikilia tu imani hiyo, hilo tu ndilo linalohitajika. Sasa, ijaze kwa shangwe na imani. Maana, atarudi pamoja na wengine watano, ama wengine saba, wabaya zaidi. Unaona? Kaa tu papo hapo na kusema, "Ninaamini. Hilo lilitosha."

266 Sasa, sisi tukiwa hatufahamiani, ningesema tu, kwa ajili ya mashahidi wawili. Biblia ilisema, "Kinywa cha mashahidi wawili, ama watatu," ninaamini ndivyo ilivyokuwa. Sivyo?

"Mashahidi wawili ama watatu, mashahidi watatu, kila neno na lithibitishwe."

267 Ninakusudia kuweka wakati wangu uliosalia hapa chini, nikiweza, kwenye mstari wa maombi. Kwa hiyo, sitaki kuchukua muda mwingi sana kwenye upambanuzi. Ni kwamba tu mweze kujua.

268 Jambo lingine, huyo mama anayeketi pale, akiwa na vipindi vya kizunguzungu. Havitakupata tena kama ukiamini tu. Niambieni alichogusa. Ni—niliona Nuru hiyo ikizunguka hapa kisha ikaenda moja kwa moja huko kwenye kona ile. Nilimwona huyo mwanamke akishikilia kichwa chake, namna *hii*, katika ono, akienda huku na huku, namna *hiyo*. A-ha. Mnaona? Alifanya nini? Aligusa vazi Lake. Sio . . . Biblia ilisema, kwamba, "Yeye ni Kuhani Mkuu" (hiyo ni kweli?) "anayeweza kuguswa na mambo ya udhaifu wetu." Hivyo ndivyo yeye alivyofanya. Mnaona jinsi alivyoitikia upesi? Hapo lilitendeka. Mnaona? Aminini tu. Sasa, hiyo inapaswa kulitatua lote. Hiyo inalifanya kweli.

269 Sasa, mnaona ni kwa nini siharakishi kupitia kwenye mstari. Ninajaribu tu kujizuia, kabisa, maana ninataka mstari mwingine kesho usiku. Bali ili tu muone ya kwamba Yeye amejitokeza jukwaani. Huyo ni Yeye. Haiwezi kuwa ni mimi. Sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu; sijui lolote kumhusu. Mnaona?

270 Ni rahisi sana, mpaka watu wakubwa wenye akili siku hizi wanayumbayumba moja kwa moja juu ya urahisi kama huo. Mnaona? Hiyo ndiyo sababu wanalikosa. Wanajaribu kulielewa. Huwezi kulielewa. Unaliamini. Unaliamini tu.

271 Huyo msichana wa Kihindi, anayeumwa na kichwa, kama angeliamini tu, kingemwacha, pia. Sijawahi kumwona. Yeye hata . . . Mnaona? Mnaona?

272 Mguse. Mguse tu, mara moja, uone kama si kweli. Unaona?

273 Watu hao ni wageni. Mwulizeni mama huyo. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Hiyo ni kweli, mbele za Mungu, kama nijuavyo. Mnaona? Mnaona? Yuko jukwaani, kama unaweza kumwamini. Lakini usiyumbayumbe tu kwake; amini. Itafanya jambo fulani kwako kama utaamini. Yeye atakuponya. Ninyi nyote mnaweza kuponywa kama tu mkiamini.

274 Mnaona, huyu hapa mwanamke amesimama jukwaani. Naye Roho Mtakatifu anasogea kule kupitia kwenye kusanyiko, akiwaponya watu, inaonyesha kwamba Yeye yuko kila mahali, yuko kila mahali, anajua yote, na yuna nguvu zote. Amina. Utukufu! Mwamshe Yesu, ndani yako. Acha Yeye ambaye amekuja ndani yako, katika umbo la Roho Mtakatifu, apitie ndani yako.

275 Sikujui, bali Mungu anakujua. Bwana Mungu anaweza kunifunulia jambo fulani lililokuleta hapa. Ungeniamini, sivyo? Vema. Nitazame. Ni—ninamaanisha kwa jambo hilo, kama vile Petro na Yakobo, mwajua, walivyosema, "Tutazame sisi." Kukuondoa tu kwenye . . .

276 Inakuja tu kutoka kila mahali. Ninaamini kutakuwako na ibada halisi ya uponyaji katika dakika chache. Mnaona? Mnaona? Mnaona?

277 Jambo moja, macho yako yanakusumbua. Karibu unakuwa kipofu. Mishipa ndani ya macho inakufa.

278 Mara ya kwanza, nilishika hilo, katika muda mrefu. Mtu fulani alisema, "Alibahatisha hilo." Sikulibahatisha. Sikulibahatisha. Sasa, kumbukeni, ninayashika mawazo yenu hapa kwa Roho Mtakatifu.

279 Hebu tuone kama nilibahatisha. Angalia hapa, dada. Wewe ni mwaminio. Una tatizo la kifua chako; kansa, kansa ya ngozi nyuma ya shingo. Sasa, unaamini Mungu ataiondoa? [Huyo Dada anasema, "Ndiyo, bwana."—Mh.] A-ha. Unataka kurudi huko New Mexico, ulikotoka, ukiamini Mungu alikuponya? Vema, Bibi Watkins, rudi . . .? . . . kule. Ponywa katika Jina la Bwana Yesu Kristo.

Unaweza kuamini. Kuwa tu na imani.

280 Hatufahamiani mmoja na mwenzake. Umeniona mikutanoni. Lakini, ninamaanisha, kukujua wewe, kusema tu ninakujua, sikujui.

281 Sasa, kidogo tu. Nimepitisha wakati wangu kwa mbali, bali hakika ninyi mnajua Yeye yupo hapa. Mwanamke huyu anayesimama hapa, tena, halafu tuta—tutawaombea. Nafikiri hao ni angalau watatu. Sivyo? Loo, naam. Hiyo ni kote kupitia kwenye kusanyiko, basi.

282 Sina habari. Unaonekana mwenye afya na nguvu, kwangu mimi. Sikujui, bali Mungu anakujua. Lakini kuna kitu fulani moyoni mwako. Ni kitu unachotamani. Na ni kwa ajili ya mtu mwingine. Ninamwona kijana mwanamume, la, vijana wawili wanaume. Ni wanao. La, mmoja wao ni mwanao, na huyo mwingine in mkweo. Na wote wawili wana tatizo la tumbo. Na wote wawili wana vivuli vyeusi juu yao. Hao, wote wawili, ni wenye dhambi. Hiyo ni BWANA ASEMA HIVI. Unaamini sasa?

Ni wangapi watakaoamini pamoja naye? Na tuombe.

283 Bwana Yesu, tunakuamini Wewe sasa kwa ajili ya haja hii, kwa ajili ya dada yetu. Ninambariki katika Jina Lako. Naomba aende na apokee yale aliyoomba, kwa ajili ya utukufu Wako. Amina.

284 Ninyi nyote mnaamini sasa kwa moyo wenu wote?

285 Sasa, njoo huku. Unaamini Yeye anaweza kuniambia shida ni ipi? Hilo si lingekuwa ni zuri, maskini tatizo hilo la pumu lingeondoka, nawe ungeweza kwenda nyumbani, uwe mzima? Vema, kama unaamini, litaondoka.

286 Unazungumza Kiingereza? Ugonjwa wa moyo, tatizo la tumbo. Mwamini Bwana Yesu na utakuacha. Amina. Vema.

287 Njoo, mama. Unazungumza Kiingereza? Vigumu kupumua; pumu. Nenda, amini. Pumua! Liamini, katika Ji—Jina la Bwana Yesu.

288 Njoo. Unazungumza Kiingereza? Unaniamini mimi kuwa ni nabii wa Mungu? Shida yako iko mgongoni mwako. Amini! Hautakusumbua tena.

289 Unaniamini mimi kwamba ni mtumishi Wake? Unasumbuliwa na baridi yabisi. Ninakuona ukijaribu kutoka kitandani. Ni vigumu kwako kufanya hivyo, asubuhi. Nenda, amini, na haitakubidi kufanya hivyo tena, nawe utakuwa mzima.

290 Mnaamini? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Moyo wako wote? ["Amina."] Mwamshe Yesu, ndani yako sasa. Kristo yupo hapa. Yuko jukwaani. Mnaamini hilo nyote? ["Amina."]

291 Sasa wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Wekeaneni tu mikono ninyi kwa ninyi sasa.

292 Ninaenda kunukuu Maandiko. Yesu alisema, "Enendeni ulimwenguni kote," Tempe, Arizona, "mkaihubiri Injili. Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; wakishika nyoka ama kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya."

293 Sasa, huku Yesu akiwa yupo sasa, kama mnaamini Yeye yupo, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Roho yule yule aliyekuwa ndani ya Yesu Kristo yupo hapa katika kanisa hili usiku wa leo.

294 Sasa, wewe mwombee huyo mtu uliyemwekea mikono. Omba tu moja kwa moja, useme, "Bwana Mungu, mponye mtu huyu." Wao wanakuombea.

295 Bwana Yesu, ninaomba, Mungu, ya kwamba Wewe utatuma nguvu Zako na Roho juu ya kusanyiko hili, juu ya maskini mwanamke huyu hapa, Bwana, aliye na barakoa hii juu ya uso wake. Ninaomba ya kwamba utawaponya, Bwana. Jalia ibilisi, dhoruba, zikomeshwe, na nguvu za Mungu zichukue mamlaka juu ya kusanyiko hili na kuondoa kila nguvu chafu na kutokuamini.

63-0117 Kumwamsha Yesu
Full Gospel Church
Tempe, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org